# HOTUBA YA WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA

# MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA (MB.),

# AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2014/2015

# YALIYOMO


ORODHA YA VIFUPISHO ........................................................ iv

DIRA ........................................................................ vii

DHIMA ........................................................................ vii

MAJUKUMU YA WIZARA ........................................................ vii

ORODHA YA VIELELEZO ........................................................ ix

1.0 UTANGULIZI ........................................................ 1

2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MIPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2013/2014 ........................................................ 4

2.1 MALENGO NA MIPANGO YA MWAKA 2013/2014 ................ 4

2.2 MAPATO ........................................................ 8

2.3 SEKTA YA VIWANDA ........................................................ 8

2.3.1MIRADI YA KIMKAKATI ........................................................ 11

2.3.2UENDELEZAJI VIWANDA VYA KIMKAKATI CHINI YA NDC ........................................................ 12

2.4 SEKTA YA BIASHARA ........................................................ 31

2.5 UENDELEZAJI MASOKO ........................................................ 38

2.6 UKUZAJI NA UENDELEZAJI UJASIRIAMALI ...................... 40

2.7 UWEKAJI MAZINGIRA BORA YA UFANYAJI BIASHARA ..... 42

2.8 UENDELEZAJI UTAFITI NA MAENDELEO ......................... 45

2.9 USIMAMIZI WA SERA NA SHERIA KATIKA BIASHARA....... 50

2.10UENDELEZAJI WA TAALUMA YA BIASHARA .................... 56

3.0 MAENDELEO YA RASILIMALI WATU ................................ 57

4.0 USIMAMIZI WA MAPATO NA MATUMIZI ............................ 58

5.0 USIMAMIZI WA UNUNUZI.................................................. 58

6.0 HUDUMA ZA SHERIA ........................................................ 59

7.0 MAMBO MTAMBUKA......................................................... 59

8.0 CHANGAMOTO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA................ 61

9.0 MALENGO YA MWAKA 2014/2015 .................................... 62

9.1 SEKTA YA VIWANDA ......................................................... 62

9.2 SEKTA YA VIWANDA VIDOGO NA BIASHARA NDOGO....... 64

9.3 SEKTA YA BIASHARA ........................................................ 65

9.4 SEKTA YA MASOKO ........................................................... 66

9.5 TAASISI CHINI YA WIZARA................................................ 67

9.5.1 MAMLAKA YA MAENEO MAALUM YA KUZALISHA BIDHAA ZA KUUZA NJE (EPZA) ..................................................... 67

9.5.2 SHIRIKA LA MAENDELEO LA TAIFA (NDC)..................... 67

9.5.3 KITUO CHA ZANA ZA KILIMO NA TEKNOLOJIA VIJIJINI (CAMARTEC) ..................................................................... 69

9.5.4 SHIRIKA LA UHANDISI NA USANIFU WA MITAMBO (TEMDO) .......................................................................... 70

9.5.5 TAASISI YA UTAFITI NA MAENDELEO YA VIWANDA (TIRDO) ............................................................................ 71

9.5.6 SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS) ......................... 72

9.5.7 BARAZA LA USHINDANI (FCT) ........................................ 74

9.5.8 WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI (BRELA) ........ 74

9.5.9 TUME YA USHINDANI (FCC) ........ 76

9.5.10 BARAZA LA TAIFA LA UTETEZI WA MLAJI (NCAC) ........ 76

9.5.11 BODI YA LESENI ZA MAGHALA (TWLB) ........ 77

9.5.12 SHIRIKA LA KUHUDUMIA VIWANDA VIDOGO (SIDO) ... 78

9.5.13 CHAMA CHA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA) ........ 79

9.5.14 MAMLAKA YA BIASHARA TANZANIA (TANTRADE) ........ 79

9.5.15 WAKALA WA VIPIMO (WMA) ........ 80

9.5.16 KITUO CHA BIASHARA CHA TANZANIA DUBAI-(TTC-DUBAI) ........ 82

9.5.17 KITUO CHA BIASHARA CHA TANZANIA LONDON (TTC-LONDON) ........ 83

9.5.18 CHUO CHA ELIMU YA BIASHARA (CBE) ........ 84

10.0 SHUKRANI ........ 84

11.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2013/2014 ........ 85

11.1 MAPATO YA SERIKALI ........ 85

11.2. MAOMBI YA FEDHA ........ 85

11.2.1 MATUMIZI YA KAWAIDA ........ 85

11.2.2 MATUMIZI YA FEDHA ZA MAENDELEO ........ 86

12.0 HITIMISHO ........ 87

VIAMBATISHO ........ 88

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ACT | Agricultural Council of Tanzania |
| AGOA | African Growth and Opportunity Act |
| BRELA | Business Activities Registration and Licensing Agency |
| CAMARTEC | Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology |
| CBE | College of Business Education |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CHC | Consolidated Holdings Corporation |
| COMESA | Common Market for Eastern and Southern Africa |
| COSOTA | Copyright Society of Tanzania |
| COSTECH | Commission for Science and Technology |
| CTI | Confederation of Tanzania Industries |
| DANIDA | Danish International Development Agency |
| DASIP | District Agricultural Sector Investment Project |
| DFID | Department for International Development |
| DIT | Dar es Salaam Institute of Technology |
| EAC | East African Community |
| EBA | Everything But Arms |
| EPA | Economic Partnership Agreement |
| EPZ | Export Processing Zone |
| EPZA | Export Processing Zone Authority |
| EU | European Union |
| FCC | Fair Competition Commission |
| FCT | Fair Competition Tribunal |
| GDP | Gross Domestic Product |

| | |
|---|---|
| GTEA | General Tyre East Africa |
| ICGI | Industrial Credit Guarantee Initiative |
| IDSL | Industrial Development Support Loan |
| IFAD | International Fund for Agricultural Development |
| JBC | Joint Border Committee |
| JICA | Japan International Cooperation Agency |
| KCB | Kilimanjaro Cooperative Bank |
| KNCU | Kilimanjaro Native Cooperative Union |
| KOICA | Korea International Cooperation Agency |
| LAT | Leather Association of Tanzania |
| MOWE | Month of Women Entrepreneurs |
| MUVI | Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini |
| MVIWATA | Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania |
| NDC | National Development Corporation |
| NEDF | National Entrepreneurship Development Fund |
| NEMC | National Environment Management Council |
| NMB | National Microfinance Bank |
| NMDF | National Marketing Development Forum |
| NTBs | Non Tariff Barriers |
| ODOP | One District One Product |
| OPRAS | Open Performance Review and Appraisal System |
| OSBP | One Stop Border Post |
| PPP | Public Private Partnership |
| RLDC | Rural Livelihood Development Company |
| SADC | Southern African Development Community |
| SEZ | Special Economic Zone |
| Sida | Swedish International Development Agency |
| SIDO | Small Industries Development Organization |
| SMEs | Small and Medium Enterprises |

| | |
|---|---|
| TAGMARK | Tanzania Agricultural Marketing Development Trust |
| TAHA | Tanzania Horticulture Association |
| TanTrade | Tanzania Trade Development Authority |
| TBS | Tanzania Bureau of Standards |
| TCCIA | Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture |
| TCIMRL | Tanzania China International Mineral Resources Limited |
| TEMDO | Tanzania Engineering, Manufacturing and Design Organization |
| TFDA | Tanzania Food and Drug Authority |
| TIB | Tanzania Investment Bank |
| TIRDO | Tanzania Industrial Research and Development Organization |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| TTIS | Tanzania Trade Integrated Strategy |
| TWLB | Tanzania Warehouse Licensing Board |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UNCTAD | United Nations Conference on Trade and Development |
| UNDP | United Nations Development Programme |
| UNIDO | United Nations Industrial Development Organization |
| USAID | United States Agency for International Development |
| WMA | Weights and Measures Agency |
| WTO | World Trade Organization |

## DIRA

Taasisi shindani, inayokwenda na wakati katika kujenga mazingira wezeshi ya kibiashara ya ndani na kimataifa katika maendeleo ya viwanda, biashara na sekta binafsi ili kuwa na uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025.

## DHIMA

Kuweka mazingira wezeshi na endelevu kwa ajili ya ukuaji wa Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo kupitia sera na mikakati madhubuti; kuwezesha ushiriki wa Sekta Binafsi; kuendeleza ujasiriamali na kuwezesha kupanuka kwa wigo wa uzalishaji, huduma na masoko ili kuongeza ajira, kipato na kuboresha maisha.

## MAJUKUMU YA WIZARA

Wizara ya Viwanda na Biashara imeundwa kwa Tamko la Serikali Na.494 la tarehe 17 Disemba, 2010, na ina dhamana ya kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera za Maendeleo ya Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Majukumu mahsusi ya Kisekta ni:-

i) Kuandaa, kuratibu na kupitia Sera na Mikakati ya Sekta;

ii) Kufuatilia na kuperemba (Monitoring and Evaluation - M & E) utendaji katika sekta.

iii) Kubuni na kuandaa programu za kuendeleza sekta;

iv) Kukusanya, kuchambua, kutathmini na kusambaza taarifa za sekta;

v) Kukuza na kuhamasisha biashara ya ndani na nje;

vi) Kuimarisha utafiti wa maendeleo ya Sekta ya Viwanda;

vii) Kuimarisha ufanisi wa utendaji wa wafanyakazi wa Wizara na Taasisi zake;

viii) Kuboresha upatikanaji wa huduma za kuendeleza biashara;

ix) Kusimamia utendaji wa taasisi zilizo chini ya Wizara;

x) Kusimamia utekelezaji wa sheria zinazosimamia viwanda, biashara na masoko;

xi) Kuboresha mazingira ya utendaji kazi za sekta binafsi; na

xii) Kutafuta fursa za masoko ya bidhaa na huduma za Tanzania.

# ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na.1: Mwenendo wa Sekta ya Viwanda na Mchango wa Sekta Katika Pato la Taifa (2002 –2013)

**HOTUBA YA WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA, MHESHIMIWA DKT. ABDALLAH O. KIGODA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA**

## 1.0 UTANGULIZI

***1. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara tarehe 03 Mei, 2014, huko Bagamoyo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2014/2015.

***2. Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia karama na afya njema inayotuwezesha leo kutekeleza majukumu ya Taifa kwa ustawi na manufaa ya Watanzania wote. Napenda kumshukuru kwa njia ya pekee Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniamini na kuendelea kunipa dhamana ya kusimamia sekta hii muhimu na nyeti katika Taifa letu. Kipekee kabisa, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa kusimamia kwa makini sana mchakato wa kuandaa Katiba Mpya ya Taifa letu. Utulivu na uvumilivu wake katika kusimamia mchakato wa uandaaji Katiba Mpya umeonesha ni kwa nini kiongozi wetu anaheshimika mno duniani. Napenda kutumia fursa hii kumuahidi Mheshimiwa Rais kuwa nitaendelea kusimamia kwa umakini mkubwa dhamana niliyopewa ili kuleta matokeo yaliyokusudiwa.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** naipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara inayoongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa (CCM) na Makamu wake, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga (CCM), na Wanakamati wote kwa ushauri wao na maelekezo murua yaliyochangia katika kukuza na kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara. Napenda kuwahakikishia Wajumbe wa Kamati hii kuwa, ushauri wenu umezingatiwa katika kuboresha Hotuba ninayoiwasilisha.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini (CCM), kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu, kwa ushirikiano tunaoupata katika kubuni na kupitisha Miswada ya Sheria na Bajeti ya Wizara. Wizara itaendelea kudumisha ushirikiano huo ili kutekeleza inavyostahiki majukumu ya sekta ya Viwanda na Biashara na Taifa kwa jumla.

6. ***Mheshimiwa Spika***, namshukuru na kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Katavi (CCM), Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa hotuba yake iliyosheheni maelekezo mazuri, yanayotoa dira na mwelekeo wa utekelezaji wa Mipango na Programu za Serikali ya Awamu ya Nne kwa mwaka 2014/2015. Aidha, nawapongeza Mawaziri walionitangulia kuwasilisha hoja zao hapa Bungeni.

***7. Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwapongeza, Mhe. Dkt. Asha-Rose Migiro (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Godfrey William Mgimwa (Mb.), na Mhe. Ridhiwan Jakaya Kikwete (Mb.), kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Majimbo ya Kalenga na Chalinze mtawalia. Pia nawapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa na Mhe. Rais kuwa Mawaziri na Naibu Waziri kuongoza Wizara mbalimbali.

***8. Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii adhimu kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Handeni kwa kuendelea kunipa moyo na ushirikiano mzuri unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu kama Waziri na pia Mwakilishi wa Jimbo la Handeni katika Bunge lako Tukufu. Naishukuru pia familia yangu hususan mke wangu, watoto, ndugu na marafiki kwa dua zao na ushirikiano wao mzuri.

***9. Mheshimiwa Spika,*** nawashukuru pia viongozi na watendaji wa Wizara, Taasisi za Serikali na wadau wote, hususan Asasi za Sekta Binafsi zikiwemo Chama cha Wadau wa Ngozi Tanzania-LAT; Baraza la Kilimo Tanzania-ACT; Baraza la Taifa la Biashara-TNBC; Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania-CTI; Chama cha Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Kilimo Tanzania-TCCIA; Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania-TPSF; Chama cha Wafanyabiashara Wanawake-TWCC na Vikundi vya Biashara Ndogo (VIBINDO) kwa michango yao katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara. Nawashukuru pia wananchi wote, waandishi na wamiliki wa vyombo vya habari kwa mchango wao mkubwa katika kuelimisha umma wa Watanzania kuhusiana na utendaji wa Wizara na uendelezaji wa Sekta ya Viwanda na Biashara, na hususan katika kuvutia uwekezaji na kuhimiza uzalishaji viwandani. Ni matumaini yangu kuwa, ari na ushirikiano huo utaendelezwa.

***10. Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii ni matokeo ya uratibu na ushirikiano mzuri wa Naibu Waziri, Mhe. Jannet Z. Mbene (Mb.); Katibu Mkuu, Bw. Uledi A. Mussa, Naibu Katibu Mkuu, Bibi. Maria H. Bilia; na Wakuu wa Idara, Vitengo, Taasisi na watumishi wote wa Wizara. Nawapongeza sana kwa kazi hii nzuri na hasa kwa kuongoza na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya kisekta. Napenda kuwashukuru pia wale wote tulioshirikiana kwa namna moja au nyingine katika maandalizi ya hotuba ninayoiwasilisha leo hii. Namshukuru pia Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na wachapishaji wengine kwa kuchapisha machapisho ya Wizara yangu kwa wakati.

***11. Mheshimiwa Spika,*** naomba kuwapa pole ndugu na jamaa kwa kuondokewa na wapendwa wetu, Mhe. William Augustao Mgimwa, aliyekuwa Mbunge wa Kalenga (CCM), na Mhe. Saidi Ramadhani Bwanamdogo aliyekuwa Mbunge wa Chalinze (CCM). Mwenyezi Mungu awarehemu na awapumzishe kwa amani, Amina.

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MIPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2013/2014

### 2.1 MALENGO NA MIPANGO YA MWAKA 2013/2014

***12. Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba kuwasilisha mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2013/2014. Kama nitakavyoainisha katika Hotuba hii, kumekuwa na kasi kubwa ya uwekezaji katika Sekta ya Viwanda na Biashara nchini kwa mwaka 2013/2014 na katika Serikali ya Awamu ya Nne kwa ujumla.

***13. Mheshimiwa Spika,*** mafanikio makubwa yaliyopatikana katika uendelezaji viwanda na biashara ni matokeo ya kuzingatia misingi ya malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II); KILIMO KWANZA; Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16); Mpango Elekezi wa Mwaka 2011 – 2025; Mpango Mkakati wa Wizara 2011/12 – 2016; na Matokeo Makubwa Sasa!

***14. Mheshimiwa Spika,*** wakati wa vita baridi, baina ya Nchi za Magharibi na Nchi za Kijamaa, tuliaminishwa kuwa ***Siasa ni Uchumi.*** Dhana hii hivi sasa imeachwa na badala yake dhana mpya inayotamalaki katika medani ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa ni ***Uchumi ni Siasa***. Mathalan, tunashuhudia nchi tajiri na zilizoendelea duniani, pamoja na siasa zao kutokuwa bora kuliko zetu, zinavyoheshimiwa kutokana na nguvu za kiuchumi zilizonazo. Hivyo, mataifa yenye uchumi duni na usiogusa kila tabaka la jamii yataendelea kuyumba kisiasa. Kwa mantiki hiyo, ningependa kulitanabaishia Bunge lako Tukufu kuwa, uchumi unaogusa kila mtu katika Taifa, kuanzia wale wenye vipato vya chini, vya kati na vya juu, vijijini na mijini, msingi wake lazima ujengwe juu ya viwanda na biashara.

***15. Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa Viwanda na Biashara katika uchumi wa Taifa, Wizara yangu katika mwaka 2013/2014, ilipanga kutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Kuendeleza na kuwezesha uwekezaji katika Viwanda Vikubwa na vya Kimkakati, hususan Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma Chuma wa Liganga na Mchuchuma na Maganga Matitu; Kiwanda cha

Viuadudu; Magadi Soda-Engaruka; Umeme wa Upepo-Singida na wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Ngaka;

ii. Kuendeleza Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (Export Processing Zones-EPZ) na Kutenga Maeneo Maalumu ya Uwekezaji (Special Economic Zones-SEZ);

iii. Kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Nguo na Mavazi; Ngozi na Bidhaa Zake;

iv. Kuhamasisha uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vinavyoongeza thamani ya mazao ya kilimo;

v. Kuendeleza na kukuza biashara ya ndani na mauzo nje

vi. Kuimarisha ushirikiano baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa ili kupanua soko la bidhaa za Tanzania husussan katika masoko ya upendeleo;

vii. Kujenga na kuimarisha miundombinu ya masoko na mifumo ya uendeshaji masoko nchini;

viii. Kusimamia na kuratibu sheria na taratibu za kibiashara kupitia taasisi zetu za usimamizi wa ubora na viwango vya bidhaa, ushindani ulio wa haki na ulinzi wa walaji;

ix. Kukuza na kuendeleza ujasiriamali na biashara ndogo;

x. Kuimarisha Taasisi za Utafiti na Maendeleo; na

xi. Kuendeleza raslimali watu.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo hayo ya kipaumbele katika uendelezaji Sekta ya Viwanda kwa mwaka 2013/2014, yamezingatia ujenzi wa Sekta ya Viwanda Shirikishi (Inclusive Industrialization) kama ilivyoainishwa katika Mkakati Unganishi wa Maendeleo ya Viwanda, na pia Viwanda Vikubwa na vya Kimkakati vitakavyowezesha ukuaji wa uchumi kwa kuhamasisha tija na uwekezaji katika sekta nyingine za kiuchumi na huduma katika Taifa. Mwelekeo huo wa ukuzaji viwanda ni matokeo ya tathmini iliyofanywa na Wizara yangu mwaka 2011, inayoonesha mchanganuo ufuatao wa aina ya viwanda vilivyopo nchini:

(a) Asilimia 88 ya viwanda Tanzania ni vidogo sana (micro industries);

(b) Asilimia 10.5 ni viwanda vidogo (small scale industries);

(c) Asilimia 0.2 ni viwanda vya kati (medium scale industries); na

(d) Asilimia 0.4 ni viwanda vikubwa (large scale industries).

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** hii ina maana kwamba, asilimia 99.6 ya viwanda nchini bado ni vichanga na kwa misingi hiyo viwanda hivyo vinahitaji kujengewa uwezo ili viweze kukua na kuzalisha bidhaa zitakazoweza kushindana katika soko la ndani na la nje ya nchi. Aidha, kati ya viwanda vyote vilivyoko katika sekta ya uzalishaji, ni asilimia 21.6 tu ndivyo vilivyoko katika sekta rasmi, wakati asilimia 78.4 viko katika sekta isiyo rasmi. Hivyo, ***Mheshimiwa Spika,*** katika kufanya mapitio ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2013/2014, nitaelezea mafanikio yaliyofikiwa katika maeneo hayo na jinsi gani Wizara inavyojaribu kuzingatia haja ya ushiriki wa Watanzania wengi zaidi katika Sekta ya Viwanda na Biashara ili kuinua kipato chao na kuwaondolea umaskini.

## 2.2 MAPATO

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi 40,330,000, kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni (tender documents), ada za leseni, faini za leseni na malipo ya malimbikizo ya madeni. Hadi kufikia Aprili, 2014, kiasi cha Shilingi 4,379,226,451 kilikuwa kimekusanywa. Ongezeko hilo linatokana na uamuzi wa Serikali kuanza kutekeleza Sheria ya Fedha ya mwaka 2011 iliyopitisha utaratibu wa kutoza ada za leseni. Utekelezaji wa Sheria hiyo ulianza mwezi Julai 2013 wakati Bajeti ya Wizara imekwishapitishwa.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili, 2014, Wizara ilikuwa imepokea Shilingi 60,585,643,352, sawa na asilimia 56 ya fedha zilizotengwa kwa Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2013/2014. Kati ya fedha hizo, Shilingi 19,509,149,056 ni za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 41,076,494,296 ni za Matumizi ya Maendeleo. Katika Shilingi 19,509,149,056 fedha za Matumizi ya Kawaida zilizopokelewa kutoka Hazina, shilingi 2,208,125,555 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi 17,301,023,501 kwa ajili ya Mishahara (PE). Vilevile, katika shilingi 41,076,494,296 za Fedha za Maendeleo zilizopokelewa kutoka Hazina, Shilingi 39,900,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 1,176,494,296 ni fedha nje.


## 2.3 SEKTA YA VIWANDA

***20.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuelezea mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka 2013/2014 napenda kutumia fursa hii kufanya mapitio ya jumla ili kuonesha mwelekeo wa

Sekta ya Viwanda katika siku zijazo. Kwanza, ukuaji wa Sekta ya Viwanda ni mzuri, kwani umeongezeka kutoka asilimia 5.5 mwaka 1998 hadi asilimia 7.7 mwaka 2013, ingawa kiwango hicho cha ukuaji kiko chini kidogo ikilinganishwa na mwaka 2012. Ukuaji huo umechangiwa kwa kiwango kikubwa na kuimarika kwa uzalishaji viwandani, hususan viwanda vya vinywaji, saruji, bidhaa za chuma; na usindikaji wa mazao ya kilimo. Hata hivyo, ongezeko la ukuaji huo, bado liko chini ya lengo la asilimia 15 la Dira ya Taifa ya Maendeleo (Vision 2025). ***(Jedwali Na. 1)***

Aidha, mwenendo wa mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa kwa kipindi rejea umekuwa ukiongezeka kwa wastani wa asilimia 9.02, kutoka asilimia 8.37 mwaka 1998 hadi asilimia 9.92 mwaka 2013. (***Kielelezo Na. 1***). Hatua zinazochukuliwa sasa na Wizara yangu na ambazo nitazieleza katika hotuba hii zinakusudia kuongeza kasi ya ukuaji wa Sekta ya Viwanda ili kuakisi malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo nayoelekeza azma ya Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kati na unaoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025. Azma hiyo inawezekana kabisa iwapo Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu wataunga mkono hatua na mikakati ya Wizara yangu.

***Kielelezo Na.1: Mwenendo wa Sekta ya Viwanda na Mchango wa Sekta Katika Pato la Taifa (1998 –2013)***




***21. Mheshimiwa Spika,*** matumaini ya kufikiwa kwa malengo tuliyojiwekea yanatokana na kuimarika kwa uzalishaji na uwekezaji katika viwanda vya msingi. Mathalan, uzalishaji wa bidhaa za chuma uliongezekai kutoka tani 46,690 mwaka 2012 hadi tani 48,312 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 3.5; na mabati kutoka tani 81,427 mwaka 2012 hadi tani 85,313 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 4.8. Aidha, uzalishaji wa saruji uliongezeka kutoka tani milioni 2.58 mwaka 2012 hadi tani milioni 3.06 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 18.9. Vivyo hivyo, uzalishaji wa bidhaa za kawaida umeongezeka. Kwa mfano, unga wa ngano kutoka tani 443,731 mwaka 2012 hadi tani 479,140 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 8.0; uzalishaji katika viwanda vya bia uliongezeka kutoka lita milioni 338.7 mwaka 2012 hadi lita milioni 359.7 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 6; na Konyagi kutoka lita milioni 16.8 mwaka 2012 hadi lita milioni 18.0 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 7.3 **(Jedwali Na. 2).**

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** ni azma yangu kuhakikisha kuwa mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Viwanda yanalindwa na kuendelezwa. Azma hiyo inawezekana kwa kuwa Wizara imedhamiria kuweka mazingira bora zaidi ya ufanyaji biashara na uwekezaji na kuendelea kutekeleza miradi ya kimkakati katika Sekta ya Viwanda.

### 2.3.1 MIRADI YA KIMKAKATI

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa miradi ya kimkakati katika Sekta ya Viwanda unafanywa na Wizara kupitia NDC na EPZA. Miradi ya Kimkakati inayotekelezwa na Wizara ni ile ambayo ama Sekta Binafsi hazivutiwi kuwekeza au ni miradi inayohitaji uwekezaji mkubwa sana lakini ni maeneo ambayo yakishughulikiwa ipasavyo yataibua uchumi na kupunguza umaskini wa wananchi wetu kwa kasi na kiwango kikubwa.

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua haja hiyo, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliendelea kutekeleza Miradi ya Uendelezaji Viwanda kulingana na malengo na mikakati tuliyojiwekea katika Mpango Unganishi wa Uendelezaji Viwanda (Integrated Industrial Development Strategy). Mpango huo unahusu uendelezaji Viwanda Mama na Viwanda vya Kimkakati (Basic and Strategic Industries); Uzalishaji wa Bidhaa za Kuuza Nje; na Kuwaunganisha Wakulima na Wenye Viwanda; na Kupanua Wigo wa Masoko Ndani na Nje ya Nchi yetu. Katika sehemu hii, maelezo yangu yatajikita katika uendelezaji viwanda. Hivyo, upanuzi wa masoko nitauelezea katika sehemu ya biashara.

### 2.3.2 UENDELEZAJI VIWANDA VYA KIMKAKATI CHINI YA NDC

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kuendeleza Viwanda Mama na vya Kimkakati, Wizara imetekeleza miradi ya kuzalisha umeme wa makaa ya mawe ya Mchuchuma na Ngaka Kusini; chuma kwa kutumia madini ya chuma cha Liganga na Maganga (Kasi Mpya); umeme kwa kutumia nguvu ya upepo huko Singida; Viuadudu vya kuua Viluwiluwi vya Mbu waenezao Malaria kibaka; Magadi na Kemikali mbalimbali kwa kutumia Magadi ya Ziwa Natron na Bonde la Engaruka.

#### (a) Liganga na Mchuchuma

***26.*** ***Mheshimiwa Spika,*** uendelezaji wa Miradi ya Mchuchuma na Liganga ulianza miaka ya 1950, kabla hata Tanzania kupata uhuru wake. Wakati wote huo, matokeo ya utafiti yalionesha kuwa miradi hiyo haina tija kiuchumi na kibiashara. Sintofahamu hiyo imepata ufumbuzi katika awamu hii ya nne ya Serikali baada ya Serikali kuamua kuwekeza katika utafiti chini ya NDC. Katika mwaka 2013/2014, utafiti huo umekamilika na kuthibitisha kuwepo kwa mashapo ya makaa ya mawe ya tani milioni 370 katika eneo la Kilometa za Mraba 30 na mashapo ya madini ya chuma ya tani milioni 219 katika eneo la Kilometa za Mraba 10. Mpango wa awali ni kuzalisha tani milioni moja za chuma na megawati 600 za umeme. Kiasi hicho cha uzalishaji wa chuma kitaifanya Tanzania kuwa ya tatu Barani Afrika katika uzalishaji chuma. Aidha, kukamilika kwa miradi hiyo kutawezesha ajira zipatazo 32,000 na mapato ya takriban shilingi 2.8 trilioni. ***Mheshimiwa Spika,*** jambo la kutia moyo ni kwamba tayari kiasi cha takriban Dola za Kimarekani 3.0 bilioni, sawa na shilingi 5.0 trilioni, zimepatikana na wabia wa miradi hiyo, yaani NDC na *Tanzania China International Mineral Resources*

*Limited (TCIMRL)* na hivyo kuwezesha ujenzi wa viwanda vya chuma kuanza mwaka 2014/2015. Napenda kutumia fursa hii kuwaomba viongozi na wananchi wa Njombe kuunga mkono juhudi hizo na hususan kufanya maandalizi ya kutumia fursa za kibiashara zitakazotokana na miradi hiyo.

**(b) Umeme wa Makaa ya Mawe (Mchuchuma na Ngaka Kusini)**

***27. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe unatekelezwa na Kampuni ya *TANCOAL Energy Limited*, ambayo ni kampuni ya ubia kati ya NDC na *Intra-Energy Company* ya Australia. Mradi huo unahusu uzalishaji wa makaa ya mawe tani milioni 2.5 kwa mwaka na umeme wa megawati 400 kwa kuanzia na Megawati 200. Kampuni hiyo ilizalisha tani 129,489 za makaa ya mawe mwaka 2013 na kuuza tani 113,693. Makaa ya mawe huuzwa kwa viwanda vya Saruji vya Tanga, Mbeya na *Lake Cement*, *Tanzania Jipsum Limited*, *Mufindi Paper Mills*, *Simba Lime*, na pia huuzwa nchi za Kenya, Malawi, Mauritius na Uganda. Aidha, katika mwaka huo, majadiliano ya mikataba ya manunuzi ya umeme na ujenzi wa msongo wa umeme (Transmission Line Agreement) yaliendelea baina ya TANCOAL na TANESCO. Mikataba hiyo inahusu ujenzi wa mitambo ya kufua umeme kiasi cha megawati 200 na ujenzi wa msongo wa umeme wa kilovolti 220 kutoka Ngaka hadi Songea ili kuunganisha na Gridi ya Taifa, umbali wa kilomita 100. Miradi hiyo inategemewa kukamilika mwaka 2018.

### (c) Kiwanda cha Viuadudu, Kibaha

***28. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia NDC inaendelea na ujenzi wa Kiwanda cha Kuzalisha Viuadudu (Biolarvicides) vya Kuua Viluwiluwi wa Mbu waenezao Malaria kwa kutumia teknolojia kutoka Cuba. Ujenzi wa majengo ya kiwanda umekamilika kwa asilimia 90 na mitambo yake imekwishanunuliwa na kufikishwa katika eneo la ujenzi na hivi sasa inawekwa tayari kwa uzalishaji mwanzoni mwa mwaka 2014/2015, yaani mwezi Julai, 2014. Aidha, katika mwaka 2013/2014, Wizara iliendeleza mazungumzo na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu kuweka utaratibu endelevu wa kuzalisha, kuuza, kusambaza na kutumia Viuadudu vitakavyozalishwa katika kiwanda hicho. Kukamilika kwa Mradi huo ni ukombozi mkubwa kwa Taifa letu katika kupambana na Malaria kwa kuwa Viuadudu vitakavyozalishwa katika kiwanda hicho kazi yake ni kuzuia mbu kuzaliana, na hivyo, kupunguza idadi ya wagonjwa wa malaria, gharama za kununua vyandarua na dawa za kuulia mbu. Matarajio ni kwamba, matumizi ya viuadudu katika miaka mitatu ya mwanzo yatapunguza sana kiwango cha kuzaliwa kwa mbu katika maeneo yatakayohusika hivyo kupunguza maambukizo ya ugonjwa wa malaria nchini. Napenda kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wote kwa jumla kuhamasisha Halmashauri na wananchi kuchangamkia matumizi ya Viuadudu katika maeneo yao.

### (d) Kiwanda cha *General Tyre Ltd (GTEA)*

***29. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Wizara iliendelea kutekeleza hatua za kukifufua Kiwanda cha Matairi cha Arusha (General Tyre Ltd-GTEA). Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) limekamilisha kukarabati majengo na ukarabati wa mfumo wa umeme unaendelea na kisha utafuatiwa na

kujaribu mitambo. Wakati huohuo, NDC imekamilisha utafiti wa soko la matairi ndani na nje ya nchi ambao ulikuwa unaangalia mahitaji ya matairi katika sehemu hizo. Utafiti unaonesha kuwa, soko lipo ambapo soko la ndani linatawaliwa na matairi kutoka nchi za Bara la Asia. Aidha, NDC inaendelea kuzungumza na wabia wenye uwezo na uzoefu wa uzalishaji wa matairi ya magari kwa lengo la kufufua na kupanua kiwanda hicho, wakati taratibu za uhamishaji wa umiliki wa mali za kiwanda kwenda NDC zikiendelea. Ufufuaji wa kiwanda hicho si tu ni muhimu katika kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana wetu na hususan wa Arusha, bali pia utawezesha uzalishaji wa mpira katika mashamba ya Kihuhwi - Muheza na Mang'ula – Kilombero kuendelezwa kwa kasi zaidi.

**(e) Umeme Utokanao na Nguvu ya Upepo (Singida)**

***30. Mheshimiwa Spika,*** Mkoa wa Singida ni miongoni mwa Mikoa nchini iliyojaaliwa kuwa na upepo mkali kiasi cha Serikali kupitia Wizara yangu kubuni mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia upepo. Mradi huo unatekelezwa kwa ubia kati ya Serikali, kupitia NDC na TANESCO, na Sekta Binafsi kupitia kampuni iitwayo *Power Pool East Africa Ltd.* Katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia NDC imekamilisha maandalizi yote muhimu ya mradi ikiwemo hati ya eneo la mradi, Mkataba wa awali wa ununuzi umeme, Cheti cha Mazingira na Leseni ya Kuzalisha Umeme. Tayari wabia wameomba mkopo nafuu wa Dola za Marekani milion 136 kutoka Benki ya EXIM ya China ili kugharamia ujenzi wa kituo cha umeme kitakachozalisha Megawati 50 na miundombinu ya kukidhi Megawati 160. Aidha, ujumbe wa maofisa wa Benki ya Exim kutoka China walitembelea eneo la mradi ili kufanya uhakiki na matarajio ni kwamba ujenzi wa mradi utaanza mwanzoni mwa mwaka 2014/2015. Faida mojawapo ya mradi huo ni

kwamba utajenga uwezo wa kitaalamu kwa Watanzania katika eneo hilo jipya katika uzalishaji umeme kwa kiwango kikubwa na pia Taifa kupata *Carbon Credit* kutokana na kuhifadhi mazingira. Kwa hiyo, nawaomba viongozi na wananchi wa Singida kutoa kila aina ya msaada kufanikisha mradi huo muhimu kitaifa.

### (f) Uzalishaii Magadi Soda (Ziwa Natron na Engaruka)

***31. Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Magadi Soda unaoendelezwa na NDC na unatarajiwa kuzalisha tani milioni moja za magadi na bidhaa nyingine za chumvi kwa mwaka. Katika mwaka 2013/2014, tafiti kuhusu wingi na ubora wa rasilimali ya magadi zilikamilika ambapo kiasi cha mita za ujazo bilioni 4.68 za magadi (brine) ambazo huongezeka kwa kiasi cha mita za ujazo milioni 1.8675 kwa mwaka zimegunduliwa katika eneo la Bonde la Engaruka. Jitihada za kumpata mtaalam mshauri wa kusanifu kiwanda cha kuzalisha magadi Engaruka na kumpata mbia atakayeshirikiana na NDC kuendeleza mradi huo zimeanza. Makadirio ya gharama za ujenzi wa kiwanda yatajulikana baada ya kukamilika kwa usanifu wa kiwanda. Mradi unatarajiwa kuanza uzalishaji mwaka 2016/2017. Mradi huo utaingiza kipato cha Dola za Marekani milioni 320 kwa mwaka na kutoa fursa za ajira 3,900. Napenda kutumia fursa hii, ***Mheshimiwa Spika***, kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kugunduliwa kwa Magadi Soda katika eneo la Engaruka kunaondoa changamoto ya wanaharakati ambao wamecheleweshwa kwa muda mrefu uendelezaji wa mradi huo muhimu katika eneo la ziwa nation utekelezaji wake utaifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazozalisha kwa wingi sana madini hayo duniani.

## MAENEO MAALUMU YA UZALISHAJI KWA MAUZO NJE (EPZ) NA UWEKEZAJI WA KIMKAKATI (SEZ)

***32. Mheshimiwa Spika,*** Wizara, kupitia EPZA, inaendelea na uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Kuzalisha Bidhaa za Kuuza Nje (*Export Processing Zones)*; na Maeneo Maalum ya Uwekezaji Kiuchumi (*Special Economic Zones)*. Mkakati huo ambao umeleta mafanikio makubwa sana ya maendeleo ya viwanda katika nchi zinazoutumia, lengo lake ni kuvutia mitaji, teknolojia za kisasa na stadi za uendeshaji (Managerial Skills). Malengo hayo niliyoyaainisha ni muhimu sana katika kujenga uchumi imara wa Taifa. Mathalan, Ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka 2011 kuhusu mchango wa Maeneo Maalum ya Uzalishaji na Uwekezaji katika maendeleo na mapinduzi ya kiuchumi ya nchi ya China inabainisha kama ifuatavyo, na naomba kununukuu,

> *"Pamoja na kwamba watunga sera, wafanyabiashara, na wanazuoni dunia nzima wamezusha mjadala wa mada ya maeneo maalum ya uzalishaji na uwekezaji (SEZ), jambo lililo dhahiri ni kwamba kuwepo kwa maeneo mengi ya aina hiyo nchini China, bila wasiwasi wowote, ndiyo injini muhimu ya hatua kubwa ya maendeleo iliyofikiwa sasa na China"*

***33. Mheshimiwa Spika,*** kulingana na Ripoti hiyo ya Benki ya Dunia inakadiriwa kuwa hadi mwaka 2007, Maeneo Maalum ya Uwekezaji (SEZ) yalichangia asilimia 22 ya Pato la Taifa, asilimia 46 ya uwekezaji toka nje, asilimia 60 ya mauzo nje, na kuwezesha ajira 30 milioni kupatikana. Ni kwa msingi huo, Wizara yangu inaweka mkazo mkubwa katika uendelezaji wa maeneo ya aina hiyo. ***Mheshimiwa Spika,***

niseme tu kuwa, uanzishwaji wa maeneo ya aina hiyo ni aghali katika hatua za awali kwa kuwa Serikali budi iwekeze? fedha nyingi katika kujenga miundombinu muhimu kama vile barabara, umeme, maji na mawasiliano. Aidha, katika baadhi ya maeneo Serikali inawajibika kuwafidia wananchi wanaoathirika katika kutekeleza dhana hiyo. Mathalan, katika kutekeleza Mradi wa *China-Tanzania Logistics Center,* Kurasini na *Mini-Tiger Plan 2020,* takriban shilingi bilioni 200 zitatumika. Lakini, kwa kuwekeza kiasi hicho cha fedha, Taifa litaweza kuvutia uwekezaji wa takriban shilingi trilioni 17.0. Ndiyo maana wakati wa kuijadili bajeti yangu katika Kamati ya Bunge tulikubaliana kimsingi kuwa Serikali ijaribu kadri iwezekanavyo kukamilisha fidia ya wananchi wa Kurasini katika Robo ya Kwanza ya mwaka 2014/2015 na vivyo hivyo fidia kwa wananchi wa Bagamoyo, Ruvuma, Mtwara na Tanga iharakishwe.

***34.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio ya hatua hizo yameanza kuonekana. Mathalan, mwaka wa fedha 2007/2008 – hadi Desemba 2013, mitaji imeongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 88 kwa mwaka hadi milioni 1,120 kufikia Desemba, 2013, sawa na ongezeko la asilimia 1,173.

***35.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (EPZA) kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, imetenga maeneo maalum ya uwekezaji katika Mikoa Ishirini (20). Jitihada zinaendelezwa za kutenga maeneo maalum katika mikoa mipya ya Simiyu, Katavi, Geita na Njombe. Katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia EPZA imeendelea kulipa fidia kwa maeneo mbalimbali nchini na hadi sasa ulipaji wa fidia katika Wilaya ya Bunda umekamilika.

***36. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia EPZA imeendelea kuweka miundombinu muhimu katika maeneo ya uzalishaji wa bidhaa kwa mauzo ya ndani na nje. Mamlaka imekamilisha ujenzi wa Kituo cha Huduma Mahali Pamoja (*One Stop Service Center*) katika Ofisi za EPZA - *Mabibo External* na tayari kuna maofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Idara ya Kazi na Ajira na Uhamiaji ambao wanatoa huduma. Kituo hicho kitarahisisha utoaji wa huduma kwa wawekezaji zikiwemo upatikanaji wa ardhi, leseni za uwekezaji na vibali vya ujenzi. Utaratibu huo umepunguza ucheleweshaji unaotokana na utoaji huduma kwa kituo kimoja kimoja na umerahisisha sana kuvutia uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi na ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (SEZ na EPZ).

***37. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, makampuni 31 yamepewa leseni za kujenga viwanda chini ya Mamlaka ya EPZ na makampuni 8 yameanza uzalishaji. Makampuni hayo yanatarajia kuwekeza mtaji wa jumla ya Dola za Marekani milioni 458 na kuajiri watu 10,276. Idadi hiyo inafanya jumla ya makampuni yanayozalisha chini ya SEZ na EPZ kufikia 98, jumla ya mtaji uliowekezwa kufikia Dola za Kimarekani bilioni 1.5 na jumla ya ajira za moja kwa moja kufikia 27,000. Hatua za awali za uendelezaji wa Bagamoyo SEZ yenye ukubwa wa hekta 9,000 umeanza. Kati ya hilo, eneo la hekta 6,500 litaendelezwa na Mamlaka ya EPZ na eneo lililobaki litaendelezwa na Kampuni ya *China Merchants Holding International Company Ltd (CMHI).* Aidha, Mpango Mpana wa eneo linaloendelezwa na Mamlaka ya EPZ umekamilika na makampuni 28 yamepewa leseni za kujenga viwanda katika eneo hilo. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu inajadiliana na Kampuni ya CMHI ili kujenga bandari ya kisasa na eneo maalum la viwanda (*Portside Industrial Zone*) katika eneo la hekta 2,500 ndani ya eneo la Bagamoyo SEZ.

***38. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha 2013/2014, Mamlaka ya EPZ kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari na TPDC, imetenga hekta 110 katika eneo la Bandari ya Mtwara kuwa "Eneo Maalum la Bandari Huru" (*Mtwara Freeport Zone*). Awamu ya kwanza ya mradi huo inahusisha eneo la hekta 10 ambalo litatumika kwa uwekezaji kutoka makampuni yanayotoa huduma kwenye Sekta ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi *(Oil and Gas Supply Base*). Mamlaka ya EPZ imekwishapata wawekezaji Saba (7) watakaowekeza katika eneo hilo.

## UWEKEZAJI WA VIWANDA VINGINE VYA SEKTA BINAFSI

***39. Mheshimiwa Spika,*** pamoja na uwekezaji unaofanyika kwa kushirikisha NDC na EPZA, Wizara imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kuhamasisha uanzishaji wa viwanda katika maeneo mbalimbali nchini, kiasi kwamba hivi sasa ni vigumu sana kupata maeneo ya uwekezaji katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. *Mheshimiwa Spika,* Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC) na Mamlaka ya EPZ imeandaa taarifa mbalimbali za fursa za uwekezaji zilizopo nchini katika miradi ya viwanda ili kuchochea kasi ya uwekezaji nchini. Katika mwaka 2013/2014, jumla ya miradi ya viwanda 120 imesajiliwa kati ya hiyo 89 ilisajili na TIC na 31 sajiliwa na EPZA. Hali hiyo imeilazimu Wizara yangu kuwaomba viongozi wote wa Mikoa na Halmashauri nchini kutenga maeneo maalum ya uendelezaji viwanda.

***40. Mheshimiwa Spika,*** aidha, Wizara pia imeanza kutafuta maeneo ya uwekezaji kupitia SIDO. Mathalan, Wizara ilipata eneo la ekari 107 kutoka Mamlaka ya Ustawishaji

Makao Makuu, Dodoma (*Capital Development Authority-CDA*) kwa lengo la kuanzisha na kuendeleza Vijiji vya Viwanda (*Industrial Villages*). Eneo hilo ni maalum kwa ajili ya kuchochea na kuvutia uwekezaji katika viwanda vya bidhaa za ngozi nchini. Tayari kazi za kupima, kuweka mipaka na kuandaa michoro/ramani ya eneo husika imefanyika na hati miliki kupatikana. Kazi kubwa iliyobaki ni kulisafisha eneo, kuweka uzio na miundombinu muhimu ili wawekezaji waweze kuingia. Aidha, Manispaa ya Singida imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 120 katika Kata ya Ng'aida kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza Kijiji cha Viwanda vya Kusindika Ngozi na Kutengeneza Bidhaa za Ngozi baada ya wananchi wa eneo hilo kuridhia. Kazi inayoendelea kwa sasa ni tathmini ya eneo hilo kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi huo. Napenda kutumia fursa hii kuwaomba viongozi na wananchi kutoa ushirikiano wa kutosha katika zoezi hilo ili liweze kukamilishwa kwa wakati.

***41. Mheshimiwa Spika,*** NDC inaendelea na ujenzi wa maeneo ya viwanda (Industrial Parks) katika Mikoa ya Kilimanjaro, Pwani, na Tanga kwa ajili ya uanzishaji wa viwanda vipya. Kazi zinazohusika na ujenzi huo ni pamoja na kugawa viwanja na kuendeleza miundombinu ya msingi kwa ajili ya uzalishaji viwandani ambayo ni barabara na mifumo ya umeme, maji safi na maji taka. Kazi zilizokamilika hadi sasa ni upimaji wa viwanja katika maeneo ya TAMCO, Kibaha (Pwani), Kange (Tanga). Ugawaji wa viwanja katika eneo la KMTC (Kilimanjaro) unatarajiwa kukamilika mwaka 2005. Aidha, NDC imekamilisha utafiti yakinifu kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya kusindika nyama katika Mikoa ya Arusha, Dodoma na Pwani. Kwa sasa, Shirika linaendelea na mazungumzo na mamlaka mbalimbali kuhusu upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya miradi hiyo. Nataraji kuwa mamlaka

husika zitatoa ushirikiano unaotarajiwa kwa kuwa utekelezaji wa miradi hiyo ni ukombozi mkubwa kiuchumi kwa wananchi wa maeneo hayo.

***42. Mheshimiwa Spika,*** katika kuthibitisha kasi ya uwekezaji katika viwanda iliyopo nchini, napenda kueleza kuwa katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani vimeanzishwa viwanda kadhaa vya Saruji kutokana na kupatikana kwa gesi asilia na pia kuwepo kwa malighafi nyingi. Miradi ambayo imekamilika na inazalisha kwa kutumia c*linker* kutoka nje ya nchi ni viwanda vya *Lee Building Materials Company Limited* kilichopo Kilwa Masoko (Lindi) na *Rhino Cement Company* kilichopo Mkuranga (Pwani). Aidha, ujenzi wa viwanda vya saruji unaoendelea ni pamoja na *Dangote Cement Co. Ltd* ulioko Mtwara-Mikindani; *MEIS Cement Company* uliopo Lindi; *Camel Cement Ltd* ulioko Mbagala, Dar es Salaam; *Lake Cement Company* ulioko Kigamboni, Dar es Salaam; *Fortune Cement Company* ulioko Mkuranga, Pwani; *Maweni Cement Company Ltd* ulioko Tanga; na *Kisarawe Cement Company* ulioko Kisarawe, Pwani. Ujenzi wa miradi inayoendelea kujengwa itakapokamilika, kwa pamoja na viwanda vilivyopo, vitakuwa na uwezo wa kuzalisha saruji isiyopungua tani milioni 6 kwa mwaka na kutoa ajira zaidi ya 5,000. Kiasi hicho cha Saruji ni mara mbili ya mahitaji ya Saruji nchini, na hivyo kuwezesha kujitosheleza kabisa. Viwanda vingine ambavyo viko katika hatua mbalimbali za ujenzi ni pamoja na Kiwanda cha Mafuta ya Kula kilichopo katika kata ya Mandawa-Singida, *Milkcom Dairies Ltd*, *Watercom (T) Ltd*-Kigamboni, *Jambo Plastics*- DSM, *Copper Leaching Plant (BMW-SEZ), Plastic Recycling Industry*-Temeke, *Metal & Plastic Industry*-DSM.

## UONGEZAJI THAMANI YA MAZAO YA KILIMO

***43. Mheshimiwa Spika,*** kwa tafsiri pana, uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo unahusu usindikaji wa mazao yatokanayo na kilimo, ufugaji, uvuvi na misitu. Katika hotuba hii nitaelezea utekelezaji kwa mwaka 2013/2014, kwa viwanda vikubwa, vya kati na vidogo. Kama utakavyoona, *Mheshimiwa Spika*, mkazo, kwa maana ya uwezeshaji wa wananchi unaofanywa na Wizara yangu, umewekwa katika viwanda vya kati na vidogo kutokana na uchanga wa viwanda vyetu niliouleza na haja ya kushughulikia mlolongo mzima wa uzalishaji (value chain) ili kuongeza tija na thamani ya mazao ya kilimo. Hivyo, mapitio ya utekelezaji nitakayoyafanya yatahusu Sekta Ndogo ya Nguo na Mavazi; Sekta Ndogo ya Ngozi na Bidhaa Zake; Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini (MUVI) na Makongano ya Uongezaji Thamani (Clusters).

### (a) Sekta Ndogo ya Ngozi

***44. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Serikali imeendelea kuimarisha Sekta ya Ngozi. Katika jitihada hizo, Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi Nchini umeendelea kutekelezwa ambapo Sekta Ndogo ya Usindikaji wa Ngozi imeongeza viwanda kutoka vitatu (3) vya awali hadi viwanda tisa (9) mwaka 2013/2014. Viwanda hivyo vina uwezo uliosimikwa (installed capacity) wa kusindika vipande vya ngozi milioni 13.2 kwa mwaka kufikia hatua ya awali (Wetblue). Kati ya hivyo, vipande vya ngozi za ng'ombe ni milioni 2.5 na vya mbuzi na kondoo ni milioni 10.7. Aidha, usindikaji umewezesha ongezeko la thamani ya ngozi zilizouzwa nje ya nchi kutoka shilingi bilioni 62.3 mwaka 2012 hadi shilingi bilioni 68.9 mwaka 2013. Vilevile, sekta hiyo imewezesha kuongezeka kwa ajira kutoka wafanyakazi 2,000 mwaka 2012 hadi wafanyakazi 2,250 mwaka 2013. Pia,

Wizara imewawezesha wadau 32 wa Sekta Ndogo ya Ngozi kushiriki Maonesho ya Kimataifa ya 37 ya SabaSaba na 14 kushiriki Maonesho ya NaneNane.

***45. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeimarisha na kuviwezesha vituo vya Mafunzo na Uzalishaji wa Bidhaa za Ngozi Dodoma, vituo vya Chama cha Wadau wa Ngozi Tanzania (*Leather Association of Tanzania-LAT*) vya Dar es Salaam na Morogoro na Chuo cha DIT - Kampasi ya Mwanza. Vituo hivyo vilitoa mafunzo ya usindikaji wa ngozi na utengenezaji wa bidhaa za ngozi kwa washiriki 351 katika mikoa tisa (9) ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza, Ruvuma, Shinyanga, na Tabora. Mafunzo yaliyotolewa yatawezesha kuzalisha bidhaa zenye ubora stahiki na shindani katika masoko ya ndani na nje.

***46. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Mawasiliano kupitia Chuo cha DIT Kampasi ya Mwanza imetoa kozi fupi katika nyanja ya usindikaji, utunzaji na uboreshaji wa ngozi (Leather Craft Tanning) kwa washiriki 39 kutoka mikoa 9 ya Tanzania Bara na Visiwani. Pia, jumla ya washiriki 93 kutoka mikoa 10 hapa nchini walihudhuria na kuhitimu katika kozi fupi ya utengenezaji viatu *(Basic Shoe Making)* na bidhaa zitokanazo na ngozi *(Leather Goods Making)*. Kutokana na chuo hicho kujengewa uwezo, kimefanikiwa kutengeneza viatu vya kijeshi zaidi ya jozi 600 kwa Taasisi ya Mafunzo wa Wanyamapori, Pasiansi-Mwanza na kusindika zaidi ya vipande 500 vya ngozi ghafi za wanyama kutoka kwa wajasiriamali. Napenda kutoa rai kwa majeshi yetu kutumia bidhaa za viwanda vyetu vya bidhaa za ngozi ili kuwajengea uwezo zaidi na kuunga mkono juhudi hizo za Serikali.

***47. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kupitia SIDO ilitambua mahitaji ya kujenga uwezo wa kusindika ngozi na kutengeneza bidhaa za ngozi kwa kuanzisha Kituo cha Mafunzo ya Ngozi mjini Dodoma, kwa kujenga jengo na kununua mashine na zana mbalimbali za kufundishia. Usimikaji wa mashine na zana hizo kwenye jengo lililopo umemaliza karibu nafasi yote iliyokuwa ikitumika kama darasa SIDO. Kwa sasa inakamilisha utaratibu wa kujenga darasa mbadala. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2010/11, Kituo kimetoa mafunzo ya kusindika ngozi kwa watu 46. Aidha, waliofundishwa kutengeneza bidhaa mbalimbali za ngozi wamefikia 127. Kati ya wahitimu wote, 50 (39%) wameweza kuanzisha viwanda vidogo vya kutengeneza bidhaa za ngozi katika maeneo yao.

**(b) Sekta ya Nguo na Mavazi**

***48. Mheshimiwa Spika,*** tangu kuanzishwa kwa Kitengo cha Kusimamia Utekelezaji wa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Nguo na Mavazi, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, tayari baadhi ya mafanikio yamekwishapatikana:

a) Kuunganisha viwanda vya nguo na mavazi ili kuwa na umoja imara na sauti moja na kuwezesha kuanzishwa kwa Tanzania Textiles and Garments Manufacturers Association of Tanzania (TEGAMAT). Kitengo kinaendelea kufanya kazi kwa karibu sana na chombo hicho katika kukabili changamoto za sekta hiyo hasa zinazohusu upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kuanzisha, kuendesha na kuendeleza viwanda vya nguo na mavazi pamoja na za uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji;

b) Kuanzishwa kwa tovuti inayoitwa www.tdu.or.tz ili kusaidia kupanua masoko ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya hapa nchini. Kila kiwanda cha nguo na mavazi kimepewa nafasi kwenye tovuti hiyo ili kujitangaza. Aidha, Kitengo kinaendelea kutoa ushawishi katika Idara mbalimbali za Serikali, Vyombo vya Ulinzi na Usalama na Magereza ili kununua bidhaa zinazozalishwa hapa nchini badala ya kuagiza nje ya nchi;

c) Kuandaliwa kwa Mwongozo wa Uwekezaji (Investment Guide) kwa ajili ya Sekta ya Nguo na Mavazi kwa lengo la kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi;

d) Waseketaji wengi wa mikono (handloom weavers) wa Dar es Salaam wameanza tena uzalishaji baada ya kuweza kupata nyuzi hapa nchini kwa bei nafuu. Uhamasishaji unaendelea kufanyika ili kufufua useketaji kwenye maeneo ya Ifakara, Iringa, Mwanza na Tabora yaliyokuwa maarufu kwa uzalishaji huo; na

e) Vikundi vya (*tie-and-dye*) na batik vilivyokuwa vinategemea vitambaa kutoka nje ya nchi, kwa sasa vinapata vitambaa bora na vya bei nafuu kutoka kwenye viwanda vya ndani.

**(c) Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini (MUVI) na Makongano ya Uongezaji Thamani (Clusters)**

***49. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Programu ya Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini (MUVI). Lengo ni kuongeza ufanisi katika mlolongo wa thamani wa bidhaa za mazao ya

alizeti, mihogo, mifugo, matunda, nyanya, mahindi, serena, ufuta, maharage na mpunga ili kuboresha kipato cha mzalishaji na kupunguza umaskini. Programu hiyo inatekelezwa katika mikoa sita kwenye wilaya 19 za Songea Vijijini, Namtumbo na Mbinga kwa Mkoa wa Ruvuma; Iringa Vijijini, Kilolo na Njombe kwa Mkoa wa Iringa; Simanjiro, Hanang na Babati kwa Mkoa wa Manyara; Sengerema, Kwimba na Ukerewe kwa Mkoa wa Mwanza; Bagamoyo, Rufiji na Mkuranga kwa Mkoa wa Pwani; na Muheza, Korogwe, Kilindi na Handeni kwa Mkoa wa Tanga. Tangu kuanzishwa mwaka 2007, Mradi umetoa huduma kwa kaya 92,910, umewezesha uanzishwaji wa miradi midogo 15,580 vijijini na kusajili vikundi vya uzalishaji 65,308. Kwa mwaka 2013/2014 pekee, zimepatikana jumla ya ajira 39,574. Kwa jumla, tathmini iliyofanyika kati ya mwezi Machi na Aprili 2014 inaonesha kuwa, Programu hiyo imekuwa na mafanikio makubwa kiasi cha Wadau wa Maendeleo kushawishika kuongeza kipindi cha programu kilichopangwa kuisha mwezi Septemba 2014. Wizara yangu inatarajia kuwa ombi letu la kuongeza muda litakubaliwa.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutumia mfumo wa uunganishaji wajasiriamali vijijini na Kongano, Wizara imeweza kuimarisha maendeleo ya viwanda vidogo na biashara ndogo na matokeo yake ni kwamba uchangiaji wake katika uchumi unaongezeka. Taarifa ya utafiti uliofanyika Mwaka 2012 (MSMEs Baseline Survey) ilionesha kuwa Mchango wa Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 27.9 na ajira zilikuwa milioni 5.2. Wizara pia imeendelea kuhamasisha uanzishaji wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo na kuimarisha ukuaji wa viwanda vidogo vilivyopo. Ni mategemeo yetu kuwa katika utafiti utakaofanyika hapo baadaye utaonesha ongezeko la mchango wa sekta katika Pato la Taifa na ajira.

***51. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na SIDO, imekuwa ikitoa mafunzo mbalimbali kwa wajasiriamali ili kuwaimarisha katika kuendesha na kuendeleza shughuli za biashara na miradi ya uzalishaji. Mafunzo yanayolenga kutoa ujuzi maalum wa kiufundi katika uzalishaji mali yalitolewa katika usindikaji wa mafuta ya kula, ngozi, chaki, ubanguaji korosho, vyakula vya mifugo, mianzi, ufinyanzi, vibuyu, kuhifadhi na kusindika vyakula vya aina mbalimbali. Kwa mwaka 2013/2014, mafunzo kama hayo yalitolewa kwa wajasiriamali 23,546. Mafunzo yaliyotolewa kwa walengwa yalilenga kujenga na kuimarisha mbinu za kibiashara na uendeshaji wa miradi ya kiuchumi hasa kuhusu usimamizi wa biashara, masoko, ubora wa bidhaa, mbinu za uzalishaji mali, utunzaji wa vitabu na mafunzo ya kutumia mashine na uongozi wa vikundi/vyama. Katika hatua zote za mafunzo, suala la viwango na ubora wa bidhaa limeendelea kupewa kipaumbele.

***52. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na SIDO imeweza kusaidia kukuza na kuboresha bidhaa za wajasirimali wadogo kwa kuwaunganisha wajasiriamali wadogo na makampuni makubwa na ya kati. Katika mwaka 2013/2014, jumla ya wajasiriamali 795 waliunganishwa na makampuni ya viwanda vya kuchambua pamba, viwanda vya kukamua mafuta ya pamba, viwanda vya bia, viwanda vya kusindika chai na viwanda vya kusindika saruji. Kazi hizo zilifanyika katika mikoa ya Arusha, Iringa, Mbeya, Mwanza, Shinyanga na Tanga. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wajasiriamali wamewezesha uzalishaji katika viwanda husika kutosimama, kudumisha ajira na kuzalisha bidhaa zenye ubora. Wajasiriamali wamewezeshwa kukuza bidhaa zao na

kupata masoko kupitia makampuni hayo.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kuhamasisha Manispaa na Halmashauri za Miji na Vijiji kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wadogo na imetembelea mikoa tisa (9) iliyohusisha Wilaya 59. Wizara pia kupitia SIDO inaendelea na maandalizi ya awali ya kujenga miundombinu ya kuanzisha Kongano ya Usindikaji wa Mafuta ya Kula kutokana na alizeti mkoani Dodoma na Singida. Vilevile, hekta 10 zimepatikana wilayani Mpwapwa kwa ajili ya kuanzisha Kongano la Karanga. Wizara inaendelea kushirikiana na wadau wengine wakiwemo TAMISEMI na Sekta Binafsi katika kutenga na kuendeleza maeneo kwa ajili ya wenye viwanda vidogo na biashara ndogo. Katika mwaka 2013/2014, tayari maeneo 23 yametengwa kwa nia hiyo.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** NDC imeanza utekelezaji wa Mpango wa Kuanzisha Kilimo cha Mashamba Makubwa ya Kibiashara na kuunganisha uzalishaji huo na usindikaji wa mazao yatakayozalishwa kwa kushirikiana na wawekezaji. Hadi sasa, Shirika limeanzisha Mradi wa Kilimo cha Michikichi kwa ajili ya kuzalisha na kusindika mafuta ya mawese katika Wilaya za Kisarawe na Kibaha Mkoani Pwani. Shamba hilo litakuwa na ukubwa wa hekta 10,000 na uzalishaji kufikia lita za mafuta 7,250 kwa hekta kwa mwaka. Aidha, mradi huo utazalisha umeme megawati 10 kutokana na mabaki baada ya kuzalisha mafuta na utaingizwa katika Gridi ya Taifa. Utekelezaji wa mradi huo unategemewa kuanza baada ya kukamilisha taratibu za kumiliki ardhi kiasi cha hekta 4,000 za awali.

***55. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhamasisha Halmashauri kutenga maeneo muafaka kwa Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Katika mwaka 2013/2014, ili kuhamasisha utengaji wa maeneo, Wizara imetembelea mikoa tisa (9) na kuhusisha wilaya 59. Ili kuandaa mwongozo utakaosaidia Mikoa kutenga maeneo mwafaka, Wizara imeanza kuhamasisha uanzishaji wa makongano ya viwanda katika kila mkoa. Kwa kuanzia, imewasiliana na Mikoa yote ili kubaini bidhaa moja au mbili zitakazohusika na kuendelezwa na kuwakilisha mkoa kwa njia ya kongano. Mikoa chini ya usimamizi wa RAS inaendelea na mchakato wa kubaini bidhaa hizo na kigezo kikubwa ikiwa ni rasilimali inayopatikana kwa wingi katika mkoa husika. Wizara itashirikiana na mikoa hiyo kuendeleza bidhaa husika kwa njia ya kongano.

**SENSA YA VIWANDA**

***56. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu inafanya Sensa ya Viwanda ya mwaka 2013/2014, ambayo ni Sensa ya nne (4) tangu nchi yetu ipate uhuru. Sensa ya kwanza ilifanyika mwaka 1961, ya pili mwaka 1978 na ya tatu mwaka 1989. Sensa hiyo inafanyika baada ya miaka 24 tangu sensa ya mwisho ilipofanyika. Kwa kawaida, sensa inatakiwa ifanyike kila baada ya miaka 10 na zoezi husika linagharimu fedha nyingi. Sensa hiyo inasaidia upatikanaji wa takwimu mbalimbali za Sekta ya Viwanda na hivyo kuwezesha Serikali kuwa na mipango na maamuzi sahihi ya kutatua changamoto za viwanda. Mafunzo ya mbinu za kufanya zoezi la kuorodhesha viwanda vyote nchini kuanzia kiwanda kinachoajiri mfanyakazi mmoja yamekwishafanyika. Zoezi la kuorodhesha linaendelea na linatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2014 na kutoa nafasi ya Sensa kamili kufanyika na kukamilika mwezi Juni, 2015.

## 2.4 SEKTA YA BIASHARA

### Mwenendo wa Mauzo na Manunuzi

***57.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Kutokana na jitihada mbalimbali za kisekta, mauzo ya bidhaa kwenye masoko ya upendeleo yamekuwa yakibadilika mwaka hadi mwaka. Mathalani, mauzo ya Tanzania kwenda Soko la Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yalipungua kutoka Dola za Marekani milioni 512.0 mwaka 2012 na kufikia Dola za Marekani milioni 419.3 mwaka 2013. Katika Soko la SADC, mauzo yalipungua kutoka Dola za Marekani milioni 1,412.3 mwaka 2012 na kufikia Dola za Marekani milioni 1,209.2 mwaka 2013. Aidha, mauzo ya bidhaa katika Soko la India yaliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 476.5 mwaka 2012 na kufikia Dola za Marekani milioni 748.2 mwaka 2013. Mauzo katika Soko la Marekani kupitia Mpango wa AGOA yalipungua kutoka Dola za Marekani milioni 66.8 mwaka 2012 na kufikia Dola za Marekani milioni 60.5 mwaka 2013.

***58.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Uagizaji wa bidhaa toka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulipungua kutoka Dola za Marekani milioni 666.8 mwaka 2012 na kufikia Dola za Marekani milioni 359.1 mwaka 2013. Soko la SADC, uagizaji ulipungua kutoka Dola za Marekani milioni 1,093.1 mwaka 2012 na kufikia Dola za Marekani milioni 835.9 mwaka 2013. Aidha, uagizaji wa bidhaa kutoka India uliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 867.4 mwaka 2012 na kufikia Dola za Marekani milioni 2,088.2 mwaka 2013. Uagizaji bidhaa kutoka Marekani ulipungua kutoka Dola za Marekani milioni 235.5 mwaka 2012 na kufikia Dola za Marekani milioni 211.9 mwaka 2013. Kwa mantiki hiyo, nchi yetu imeagiza zaidi kutoka nchi za nje kuliko kile ilichouza nje na hivyo uwiano wa biashara umekuwa hasi kwa nchi yetu. ***(Jedwali Na 3)***

Naomba nitoe rai kwa Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu kuwaomba wananchi kujiimarisha zaidi kwa kuongeza uuzaji nje na ndani wa bidhaa zilizoongezwa thamani kuliko mazoea ya kuuza mazao ghafi. Aidha, tuipende nchi yetu na kuunga mkono jitihada zake kwa kupenda zaidi mazao na bidhaa zinazozalishwa hapa nchini.

## MIKAKATI YA KUKUZA MAUZO NJE

***59.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza azma ya Serikali ya kukuza na kuendeleza mauzo nje, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la TanTrade ilitekeleza masuala yafuatayo kwa mwaka 2013/2014:-

(i) Kushiriki katika majadiliano ya kibiashara baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa kwa lengo la kupata masoko ya upendeleo katika ushuru wa forodha. Mathalan, kupitia majadiliano hayo hususan ya Duru la Doha, mbali na fursa za masoko, tumefanikiwa kupata misaada ya kifedha na kiufundi ambayo itawezesha kujenga uwezo wa watumishi kwenye masuala ya kibiashara na uwekezaji;

(ii) Kuandaa na kushiriki katika maonesho ya Kimataifa. TanTrade kwa kushirikiana na Wizara pamoja na wadau wengine iliandaa Maonesho ya 37 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam. Katika Maonesho hayo, Mamlaka iliandaa banda maalum kwa bidhaa za Tanzania likiwa na lengo la kutoa fursa ya kipekee kwa bidhaa hizo kutangazwa na kuihamasisha Jumuiya ya Wafanyabiashara wa ndani na watembeleaji kwa ujumla kutumia bidhaa za Tanzania. Kadhalika liliandaliwa banda maalum la kuonesha asali na bidhaa nyingine za nyuki. Banda hilo lilizinduliwa na

Mhe. Waziri Mkuu ikiwa ni pamoja na kuzindua mizinga iliyowekewa Kiambishi Anuai (Bar-code) kwa kushirikiana na GS1 Tanzania kwa mizinga iliyotengenezwa kwa utaalam zaidi;

(iii) TanTrade iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Maonesho ya Biashara ya Kimataifa: Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Rwanda yaliyofanyika Kigali tarehe 24 Julai – 7 Agosti, 2013, ambapo Makampuni 7 na Wajasiriamali 15 walishiriki katika Maonesho hayo; Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Nairobi yaliyofanyika Nairobi, Kenya tarehe 30 Septemba –6 Oktoba. 2013. Aidha, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Makampuni ya Konyagi pamoja na Wajasiriamali 14 walishiriki na kutangaza bidhaa na huduma za Tanzania katika soko la Kenya; na TanTrade kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini, Chama cha Wafanyabiashara wa Madini Tanzania (TAMIDA) iliandaa na kusimamia Maonesho ya Pili ya Kimataifa ya Vito na Usonara ya Arusha (The 2nd Arusha International Gem, Jewellery and Mineral Fair (AIGJMF) yaliyofanyika katika Hotel ya Mount Meru tarehe 28 hadi 31 Oktoba, 2013;

(iv) Katika kuhakikisha bidhaa za Tanzania zinapata fursa za masoko ndani ya nchi, kikanda na kimataifa, TanTrade ikiwa ni mwanachama wa "World Trade Point Federation (WTPF)" inasimamia Kituo cha Taarifa za Biashara cha Dar es Salaam (Dar es Salaam Trade Point). Kituo hicho kinawaunganisha Wafanyabiashara wa Tanzania waliojiunga nacho na wenzao katika nchi zipatazo 70 duniani kote kwa lengo la kubadilishana taarifa na fursa za biashara na uwekezaji**.** TanTrade inaendelea kuwahamasisha wafanyabiashara na Jumuiya zao kujiunga na kituo hicho kama chombo chenye manufaa kwao;

(v) TanTrade kwa kushirikiana na Wizara, na Chama cha Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Kilimo Zanzibar (ZNCCIA) iliandaa Maonesho ya Kwanza ya Idd El Hajj yaliyofanyika katika Hoteli ya Bwawani, Zanzibar kuanzia tarehe 17-20 Oktoba, 2013. Washiriki 42 kutoka ndani na nje ya nchi walionesha na kuuza bidhaa zao kwa watembeleaji. Washirki wa nje walitoka nchi za India, Malaysia, Misri na Syria. Maonesho ya Idd El Hajj yatakuwa yanafanyika kila mwaka yakiwa na lengo la kuwezesha wenye viwanda na wafanyabiashara kwa ujumla kupata masoko kwa bidhaa zao katika kipindi cha Sikukuu ya Idd El Hajj.

***60. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje ambao upo chini ya Mpango Unganishi wa Biashara, kupitia Mradi wa Enhanced Integrated Framework Tier 1 (Capacity Building for Trade Mainstreaming) tayari yameainishwa mazao ya asali na parachichi ambayo yatapewa kipaumbele ili kuweza kuyazalisha kwa ajili ya masoko ya nje. Hadidu za Rejea za kufanya utafiti ili kuweza kuzalishwa kwa wingi na kwa ubora zimekwishaandaliwa na Mshauri Mwelekezi amekwishapatikana. Utafiti huo unafanyika katika Mikoa ya Kilimanjaro (Siha) pamoja na Njombe ili kuangalia mnyororo wa thamani katika zao la parachichi na asali.

***61. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha 2013/2014, Wizara yangu imeendelea kuhamasisha Jumuiya ya Wafanyabiashara kuhusu fursa za masoko zilizopo katika masoko ya Kikanda, Kimataifa pamoja na yale ya upendeleo maalum ikiwemo AGOA na Soko la Ulaya chini ya Mpango wa Everything but Arms (EBA). Uhamasishaji na ushirikishwaji

huo umetekelezwa kwa njia ya vikao vya kazi, mikutano, maonesho ya biashara, vipeperushi, vipindi vya radio na luninga, magazeti na tovuti ya Wizara. Wizara yangu kwa kushirikiana na taasisi binafsi imeendelea kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara hao kupitia Taasisi zao zinazowawakilisha.

***62. Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu kwa kushirikiana na Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi ilishiriki katika majadiliano na nchi mbalimbali kwa lengo la kukuza biashara na uwekezaji**.** Hii ni pamoja na kuandaa mikutano kati ya Tanzania na ujumbe wa wafanyabiashara kutoka Afrika ya Kusini, China, Japani, India, Nchi za Ghuba na Uturuki. Vilevile, katika kipindi hicho, Wizara yangu imeongoza ujumbe wa wafanyabiashara katika makongamano ya kibiashara na uwekezaji katika nchi za China, India na Uturuki.

***63. Mheshimiwa spika*** majadiliano hayo yamewezesha Serikali ya Uturuki kupitia Shirika lake la ndege (Turkey Airways) kuanzisha safari za ndege kutoka Istanbul kuja Dar es Salaam. Vilevile, China ineweza kuongeza wigo wa bidhaa zinazouzwa katika soko lake chini ya mpango wa *Duty Free Quota Free* kutoka bidhaa 448 hadi 4,200. Aidha, Naibu Waziri wa Biashara kutoka Serikali ya China aliongoza ujumbe wa wafanyabiashara sabini na tano (75) ambao pamoja na mambo mengine, ujumbe huo ulikuwa na maonesho ya biashara (China Brand Show 2013) yaliyofanyika mjini Dar es Salaam katika Ukumbi wa *Diamond Jubilee.*

***64. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa majadiliano ya Kibiashara ya Kimataifa chini ya Shirika la Biashara Duniani – WTO ambapo majadiliano ya Duru la Doha yanaendelea, Wizara imeendelea kushirikiana na Ubalozi wetu Geneva na

kwa kupitia makundi ambayo sisi tunashiriki majadiliano na hasa kundi la nchi maskini, kutetea maslahi yetu. Matokeo mazuri yalipatikana katika mkutano wa mwisho wa Mawaziri wa Biashara wa nchi wanachama wa WTO uliofanyika tarehe 3-7 Desemba, 2013 mjini Bali, Indonesia. Nchi maskini ikiwemo Tanzania zilipata mafanikio yafuatayo:

i. **Kilimo:** Usalama wa chakula kwa nchi zinazoendelea na nchi changa zinaruhusiwa kununua na kuhifadhi kwa ruzuku kwa muda wa miaka 4;

ii. **Biashara ya Huduma:** WTO imetakiwa kuandaa mpango wezeshi utakaozisaidia nchi maskini wanachama wa WTO kuanza kunufaika na soko la upendeleo la Biashara ya Huduma;

iii. **Maendeleo:** Nchi tajiri wanachama wa WTO wametakiwa kutoa masoko ya upendeleo na yenye masharti nafuu kwa nchi maskini ili ziweze kujikwamua kiuchumi;

iv. **Haki Bunifu/Miliki/Hataza zinazohusiana na biashara (Trade Related Intellectual Property Rights-TRIPS):** Nchi masikini wanachama wa WTO zimeongezewa muda kutowajibika na makubaliano ya awali ya TRIPS hadi mwaka 2021, kwa nia ya kutumia muda huo kujijengea uwezo kwenye maeneo husika; na

v. **Misaada ya Biashara *(Aid for Trade-AfT)*:** Nchi Tajiri wanachama wa WTO wamekubali kutilia mkazo nia yao ya kuzisaidia nchi wanachama masikini kupitia *Aid-for-Trade* ambapo mpango mpya wa misaada hiyo umetakiwa uwe umekwishaandaliwa ifikapo mwaka 2015.

***65.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Vituo vya Biashara vya London na Dubai vimeendelea na majukumu ya kuitangaza Tanzania na kuvutia wawekezaji ikiwemo utafutaji wa masoko ya bidhaa zetu. Hata hivyo, jitihada za uwezeshaji kibajeti zinaendelea kufanywa ili Vituo viweze kutimiza majukumu yake ipasavyo.

***66.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu bado ina azma ya kuanzisha Vituo vipya vya kibiashara vya China na Afrika Kusini na pia kupeleka Waambata wa Biashara nchini Marekani na Ubelgiji kwa lengo la kuitangaza Tanzania na kutafuta masoko ya bidhaa na uwekezaji. Aidha, mawasiliano yanaendelea kufanyika kati ya Wizara yangu, Wizara ya Fedha na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ili kutimiza azma hiyo.

***67.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu na wadau wetu wameendelea kushiriki kikamilifu katika majadiliano yanayoendelea kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya. Majadiliano hayo yako katika hatua nzuri ijapokuwa kuna baadhi ya maeneo ambayo hadi sasa muafaka haujafikiwa na haswa yale yenye maslahi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa mfano, masuala ya kodi za bidhaa za kuuza nje (export tax), kutoa fursa sawa za upendeleo (Most Favoured Nation-MFN), ruzuku inayotolewa na Jumuiya ya Ulaya kwa wakulima wake (Agricultural Subsidies), kuunganisha bidhaa (Cummulation) na nchi za ACP na Afrika Kusini, masuala ya utatuzi wa migogoro (Dispute Settlement) na mwisho suala la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo. Hata hivyo, tumeendelea kunufaika na Soko la EU kwa kuuza bidhaa zetu bila kutozwa ushuru ijapokuwa Jumuiya ya Ulaya imetahadharisha kuwa iwapo hatutakamilisha majadiliano hayo na kusaini Mkataba ifikapo Oktoba, 2014, huenda itasitisha fursa hizo.

***68.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mchakato wa kuanzisha Umoja wa Forodha (Custom Union) kwa nchi wanachama wa SADC yapo katika hatua za awali. Hata hivyo, tofauti na mategemeo ya awali, majadiliano ya kuanzisha Umoja huo yanaenda taratibu ikilinganishwa na matarajio ya awali ya kukamilika kufikia mwaka 2010. Tanzania imeendelea kutekeleza Itifaki ya Biashara ya SADC na kwa sasa tuko katika hatua ya Eneo Huru la Biashara ambapo nchi kumi na mbili (12) kati ya nchi 15 wanachama wa SADC, ikiwemo Tanzania, zimeondoleana ushuru wa forodha kwenye bidhaa zinazozalishwa katika nchi wanachama na kukidhi vigezo vya uasili wa bidhaa.

***69.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wajasiriamali na wafanyabiashara wake kwa kutoa elimu ya Kanuni na Sheria za masoko ili kuzingatia ubora katika fursa za masoko ya EAC na SADC. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na asasi zinazowakilisha wafanyabiashara kama TCCIA, CTI, TPSF na TANEXA, imeendelea kuwahamasisha wafanyabiashara kuzichangamkia fursa hizo na hivyo kuchangia katika Pato la Taifa na kuongeza fursa za ajira.

## 2.5 UENDELEZAJI MASOKO

***70.*** ***Mheshimiwa Spika***, uendelezaji masoko unahusu uendelezaji miundombinu ya masoko na mfumo wa uendeshaji masoko. Kwa upande wa miundombinu, nitaelezea kwa muhtasari hatua iliyofikiwa katika kujenga masoko nchini. Aidha, Hotuba hii itahusu Mfumo wa Stakabadhi Ghalani na *Commodity Exchange*.

**Ujenzi wa Masoko Mikoani na Mipakani**

***71. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Mradi wa *District Agricultural Sector Investment Project* – DASIP, iliendelea na ujenzi wa masoko saba ya mipakani (Mtukula - Missenyi, Kabanga - Ngara, Nkwenda - Karagwe, Murongo – Karagwe, Mnanila – Buhigwe/Kasulu, Remagwe – Tarime, na Busoka- Kahama). Kati ya Masoko hayo, masoko matano ya Kahama (bandari kavu), Karagwe (Nkwenda na Murongo), Ngara (Kabanga) na Tarime (Sirari) yalikamilika mwezi Aprili, 2014. Masoko ya Mtukula (Misenyi) na Mnanila (Kasulu) imekamilisha michoro ya soko lake. Katika kuendeleza biashara mipakani, Wizara kupitia Mfuko wa Fedha wa Umoja wa Nchi za Ulaya (EDF 10) imejenga masoko matatu ya Nyamugali - Wilayani Buhigwe(Kigoma), Mkenda-Songea Vijijini (Ruvuma) na Mtambaswala - Nanyumbu (Mtwara), ambayo yote yamekamilika na yatakabidhiwa hivi karibuni kwa Halmashauri husika. Aidha, Wizara imefanya makabidhiano na Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe kwa Soko la Nyamugali ili lianze kutumika.

**Mfumo wa Stakabadhi Ghalani**

***72. Mheshimiwa Spika,*** Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ulianzishwa na Serikali ili kuvunja ukiritimba uliokuwepo katika biashara ya mazao ya kilimo. Ukiritimba huo ulisababisha mkulima kunyonywa kutokana na kupunjwa bei na wanunuzi na pia mizani iliyotumika kuwa na uwalakini kutokana na kutokuwepo usimamizi makini. Aidha, baadhi ya wanunuzi waliwafuata wakulima mashambani kwao na hivyo kuwapa bei za chini sana. Kwa ujumla, hakukuwepo ushindani. ***Mheshimiwa Spika,*** manufaa ya mfumo huo yalijionesha wazi kwenye zao la korosho ambapo wakulima kutoka mikoa ya Lindi, Mtwara na Tanga wamepata faida

kwa kuuza korosho kwa bei ya kati ya shilingi 1,000 hadi shilingi 1,350. Wakulima kutoka mikoa ya Ruvuma na Pwani wamepata hasara baada ya kuuza korosho zao chini ya bei dira ya shilingi 1,000 kwa bei ya kati ya shilingi 700 hadi shilingi 900 kutokana na kutotekeleza Mfumo wa Stakabadhi Ghalani katika maeneo hayo. Hivyo, nawaomba viongozi na wananchi tuunge mkono Mfumo huo na pia tusaidiane kutatua changamoto zilizojitokeza. Hadi sasa kumekuwepo mwitikio mzuri. Mathalan, katika mwaka 2013/2014, Bodi imetoa leseni za biashara kwa maghala 28 na waendesha maghala 17. Aidha, jumla ya tani 111,952 za korosho, tani 6,000 za kahawa na tani 700 za mpunga zilikusanywa na wakulima, vikundi vya wakulima na vyama vya ushirika vya msingi zilihifadhiwa na hatimaye kuuzwa kwa wanunuzi mbalimbali.

## 2.6 UKUZAJI NA UENDELEZAJI UJASIRIAMALI

***73. Mheshimiwa Spika,*** ili kuwawezesha wajasiriamali kukidhi mahitaji ya mikopo na kuwawezesha kupata mitambo, zana za kazi, vifaa na malighafi, katika mwaka 2013/2014, maombi 11,364 ya mikopo yaliyopokelewa yenye thamani ya Shilingi bilioni 13.091. Kati ya maombi hayo, jumla ya mikopo 13,444 ikijumulisha maombi 2,080 ya mwaka 2012/2013 yenye thamani ya Shilingi bilioni 11.309 ilitolewa. Aidha, katika mikopo iliyotolewa, asilimia 54 ilitolewa kwa wanawake na asilimia 39 ilitolewa kwa miradi ya vijijini na iliwezesha kupatikana kwa ajira 14,789 ambapo asilimia 54 zilinufaisha wanawake.

***74. Mheshimiwa Spika,*** kwa kushirikiana na wadau, Serikali imeendelea kuwawezesha wakulima kupata rasilimali fedha kwa ajili ya masoko ya mazao na bidhaa za kilimo kupitia

Benki za NMB, CRDB na TIB. Katika mwaka 2013/2014, Serikali imewezesha kuwaunganisha wakulima wa mpunga kutoka Wilaya za Misungwi, Kwimba na Magu na Benki ya NMB kwa ajili ya kupata mikopo.

***75.*** ***Mheshimiwa Spika,*** utoaji wa huduma katika karibu maeneo yote unazingatia kumjengea uwezo mjasiriamali mdogo ili kuongeza ufanisi na tija katika shughuli zake za uzalishaji au biashara. Ingawa huduma zote zinamlenga mwananchi hasa mkulima, mtazamo wa SIDO unaelekezwa zaidi katika maeneo makuu matatu yafuatayo:

a) Kujenga msingi na uwezo wa kuzalisha bidhaa kutokana na malighafi zilizopo katika kuchangia maendeleo ya viwanda vidogo vijijini (Product Development support);

b) Kujenga uwezo wa kuzalisha mitambo na zana za kilimo, kuzalisha vipuri vyake, usambazaji pamoja na ufundishaji wa watumiaji; na

c) Mafunzo ya ujasiriamali na ujuzi maalum (skills transfer, entrepreneurship, business and technical training) hasa kujenga uwezo wa kuongeza thamani mazao na mafunzo ya ujasiriamali na uongozi wa biashara.

Katika mwaka 2013/2014 (Julai – Desemba 2013), jumla ya viwanda vidogo 198 vilianzishwa na kuwezesha utengenezaji wa ajira 1,809.

***76.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kukua na kuongezeka kwa mchango wa Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo kunategemea zaidi uanzishwaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo mpya. Wizara kwa kupitia SIDO, imekuwa ikitekeleza programu ya kiatamizi ya kuwezesha wabunifu kubadilisha

mawazo yao kuwa bidhaa mpya. Chini ya utaratibu huo, jumla ya mawazo ya kutengeneza bidhaa mpya 58 yameatamiwa katika mikoa ya Dar es Salaam (28), Rukwa (7), Arusha (9), Mbeya (9) na Mwanza (5). Kati ya mawazo yaliyolelewa, 18 yamekwisha toa bidhaa mpya ambazo zimefikia hatua ya kuingizwa sokoni.

## 2.7 UWEKAJI MAZINGIRA BORA YA UFANYAJI BIASHARA

***77. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha 2013/2014, Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara za kisekta katika ujenzi wa OSBP katika mipaka mbalimbali. Ujenzi wa majengo ya Vituo vya Mipakani katika vituo vya Sirari, Wilaya ya Tarime Mkoani Mara; na Kituo cha Mtukula, Wilaya ya Misenyi Mkoani Kagera,viko katika hatua za mwisho kukamilishwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na SIDO, TIRDO, BRELA, WMA, TBS na Kampuni ya *GS1 Tz National* hutoa mafunzo ya biashara kwa Jumuiya ya wafanyabiashara mipakani.

***78. Mheshimiwa Spika,*** wizara katika kipindi cha 2013/2014, kwa kushirikiana na wadau wengine, tumewezesha kuanzishwa kwa Kamati za Pamoja Mipakani (JBCs) katika mipaka ya Mtukula, Namanga, Kabanga, Rusumo, Sirari, Kasumulo, na Tunduma ili kuwezesha Taasisi za Udhibiti mipakani kufanya kazi kwa pamoja. Lengo ni kurahisisha na kupunguza muda wa shehena za mizigo pamoja na watu kuvuka mipakani. Mpaka sasa, Kamati za Pamoja Mipakani (JBCs) katika mipaka 7 zimeanzishwa kwa jukumu la kuunganisha na kuwezesha Taasisi za Serikali na za Sekta Binafsi kuwezesha bidhaa na huduma kupita mpakani kwa muda mfupi, kuondoa vikwazo visivyo vya kiushuru (NTBs) hatua itakayopunguza gharama za kufanya biashara na kuleta ufanisi mipakani.

***79. Mheshimiwa Spika,*** marekebisho ya sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Majina ya Biashara (Sura 213); Sheria ya Makampuni (Sura 212); Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Sura 155); na Sheria ya *Merchandise Marks* (Sura 85) yalipitishwa na Bunge. Wizara kwa kushirikiana na wadau husika imetunga Kanuni za kutekeleza Sheria tajwa. Hatua za kutangaza Kanuni hizo kwenye Gazeti la Serikali zinaendelea. Aidha, Wizara inaandaa marekebisho ya Sheria zifuatazo: Sheria Na 10 ya Stakabadhi za Maghala, *"The Export Control Act", The Agricultural Products (Control of Movement) Act",* Sheria ya Haki Miliki na Haki Shiriki; Sheria ya Vipimo, Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara (BARA) na Sheria ya Ushindani. Marekebisho ya Sheria za BARA na Sheria ya Ushindani zipo katika hatua za kuandaa Muswada. Sheria ya Stakabadhi za Maghala ipo katika hatua ya kukusanya maoni ya wadau na Sheria nyingine zipo katika hatua ya uandishi wa nyaraka za Serikali.

***80. Mheshimiwa Spika,*** kulingana na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (Big Results Now) uliozinduliwa mwaka jana kwa kuhusisha sekta sita za kipaumbele ambazo ni Niashati na Gesi Asilia; Kilimo; Maji; Elimu; Usafirishaji; na Uhamasishaji wa Rasilimali, Wizara ilishiriki kikamilifu katika kutafuta nini kifanyike kupitia mfumo wa kimaabara (labs) ulitumika kuchuja aina mbalimbali za mawazo na mbinu za kutatua matatizo na changamoto (complex issues) katika kuboresha uchumi wetu kulingana na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Ijapokuwa Sekta ya Viwanda na Biashara haikuwa na *Lab* yake yenyewe, lakini kwa kuwa ni kiungo muhimu cha utekelezaji katika sekta nyingine, Wizara yetu ilishirikishwa katika *Lab* ya Sekta ya Kilimo. Kati ya maeneo ya utekelezaji wa BRN katika sekta hiyo, Wizara ya Viwanda na Biashara ina mchango katika eneo la kuendeleza masoko ya vijijini kwa kuanzisha

Collective Warehouse Marketing Systems (COWABAMA) na kuendeleza Soko la Mazao na Bidhaa (Commodity Exchange Market). Katika kushiriki utekelezaji katika maeneo kuanzisha Soko la Mazao na Bidhaa (Commodity Exchange), Wizara imeaandaa Waraka wa kuanzishwa kwa Soko hilo na suala hilo lipo katika ngazi za juu za maamuzi. Kwa upande wa uanzishwaji wa Collective Warehouse Marketing Systems (COWABAMA), ukaguzi wa hali halisi ya maghala yote katika maeneo yanayohusika umefanyika na utekelezaji wa kuanzisha maghala hayo umepangwa kufanyika katika miaka mitatu badala ya miwili ya awali, 2013/2014 2014/2015.

***81. Mheshimiwa Spika,*** pamoja na marekebisho ya Sheria mbalimbali ili kuboresha mazingira ya biashara nchini, Wizara yangu ilishiriki pia awamu ya pili ya Maabara Maalum (Lab) kuhusu Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania iliyozinduliwa rasmi na Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara, Taasisi na Sekta Binafsi inatekeleza eneo la maboresho ya Sheria hususan Uandikishaji wa Makampuni, Majina ya Biashara na upatikanaji wa leseni za biashara. Katika hatua za awali, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara, Taasisi na Sekta Binafsi imeanza kutekeleza masuala ambayo hayahitaji fedha na itaendelea kutekeleza yale yanayohitaji fedha, yenye lengo la kuboresha mazingira ya biashara nchini. Masuala hayo ni pamoja na kuanzisha *National Business Portal* itakayorahisisha uandikishaji wa Makampuni na Majina ya Biashara, Utoaji wa Leseni za Biashara kupitia njia ya mtandao (Online Registration and Business Licensing) pamoja na kuainisha aina za leseni, taasisi na wakala za uthibiti (regulatory institutions). Lengo la hatua hiyo ni kubaini sheria zinazokwaza biashara ili kuzirekebisha au kuzifuta kabisa kwa lengo la kupunguza muda wa kuanza

biashara ambao kwa sasa, kulingana na taarifa ya Benki ya Dunia, unachukua siku 26. Lengo ni kupunguza muda huo hadi kufikia siku tano na pia kupunguza taratibu za kupata leseni ya biashara kutoka siku tisa kufikia taratibu tatu. Jitihada hizo zitawezesha uandikishaji au upatikanaji wa leseni kufikia siku moja ifikapo mwaka 2016.

## 2.8 UENDELEZAJI UTAFITI NA MAENDELEO

***82. Mheshimiwa Spika,*** utafiti na teknolojia ni msingi mkuu katika kuanzisha miradi ya uzalishaji viwandani. Matumizi ya teknolojia muafaka licha ya kuongeza ufanisi, huleta tija na kuhakikisha bidhaa inakuwa na viwango vinavyotakiwa.

***83. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha 2013/2014, Taasisi za Uwekezaji, Utafiti, Maendeleo ya Teknolojia na Mafunzo zilizo chini ya Wizara (CAMARTEC, CBE, EPZA, NDC, TEMDO na TIRDO) zimetekeleza yafuatayo:

**(a) TIRDO kwa kushirikiana na wadau ikiwemo COSTECH imeendeleza**:

i. Utafiti wa kaushio la jua na majaribio ya kuboresha kaushio hilo ili kutoa bidhaa bora na zenye ushindani hususan muhogo;

ii. kutoa huduma za upimaji wa uharibifu wa mazingira unaotokana na uzalishaji wa viwandani na kutoa ushauri wa utunzaji na uhifadhi wa mazingira katika uzalishaji. Ushauri huo umetolewa katika viwanda vya tumbaku, saruji, mbao, mabati,

vinywaji na makonyo ya karafuu katika mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Mbeya, Tanga na Zanzibar;

iii. Kufanya upembuzi yakinifu na kutayarisha mpango wa ufufuaji wa Kiwanda cha Mafuta ya Makonyo kilichoko Pemba;

iv. Kufanya tathmini ya matumizi sahihi ya teknolojia katika uzalishaji na ukaushaji wa chumvi kwenye Kiwanda cha Chumvi cha Wawi, Pemba;

v. Kubuni mtambo wa kuchakata taka za ngozi *(leather recycling machine)* ambao umekwishanunuliwa na uko katika hatua ya usimikwaji;

vi. Kuhamasisha matumizi ya nembo za mistari kwa makampuni ya ndani na nje ya nchi. Mpaka sasa, makampuni 570 hapa nchini yamekuwa wanachama wa GS1 na bidhaa 10,200 zimepata nembo za mistari;

vii. Kufanya tathmini za kitaalamu (technical assessments) katika viwanda vipya sita (6) vinavyohitaji kupata mikopo kutoka Benki ya Maendeleo (TIB) ili kushauri kitaalam endapo miradi/viwanda hivyo vitafikia malengo kama benki itatoa mikopo hiyo. Viwanda vilivyofanyiwa tathmini ni viwanda vya kuzalisha sukari, *filter* za magari, majiko yanayotumia makopo *(canisters)* ya gesi ya *butane*, maji, juisi, na uzalishaji wa wanga kwa kutumia muhogo vilivyoko Dar es Salaam, Pwani na Zanzibar;

viii. Kutoa mafunzo na kufanya tathmini kwa wazalishaji wadogo waliojengewa tovuti za kutangaza bidhaa zao ili kubaini changamoto zinazowakabili na walivyoweza kufaidika na tovuti hizo. Wazalishaji wapatao 13

waliweza kuingiza bidhaa zao kwenye masoko kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara na Pwani na kupata nembo za mstari (Bar Codes) ya ndani na nje ya nchi***;*** na

ix. Kukamilisha Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi na kupitishwa na Menejimenti na Bodi ya TIRDO. Hadi sasa, Andiko la Mradi (Business Plan) limetayarishwa na upembuzi yakinifu umefanyika.

**(b) TEMDO imetekeleza shughuli zifuatazo:**

(i) Kutoa ushauri wa kihandisi pamoja na mafunzo katika viwanda kumi vya kati na vikubwa kwa lengo la kuongeza uzalishaji, ubora wa bidhaa, faida, kuhifadhi mazingira na matumizi bora ya nishati kwa *Mount Meru Millers*, *Kijenge Animal Feed, Banana Investments Ltd, Pepsi SBC (T) Ltd, Sunflag Textile Mills, A-Z Textile Mills (Arusha), TPC Ltd, Tanzania Breweries Ltd (TAMACO) (Kilimanjaro), Tandiary Ltd, Reli Assets Holding Co.* na Tanzania Railways Co. Ltd (Dar es Salaam). Huduma za ushauri na kihandisi zimetolewa kwa viwanda vya *Banana Investments Ltd* na TAMACO kulingana na mahitaji yaliyobainishwa;

(ii) Kuboresha miundombinu ya kiatamizi na kutoa huduma kwa wajasiriamali watengenezaji wa mashine na vifaa kwa matumizi ya viwanda vya kati (machinery and equipment for light industries). Wajasiriamali wanane (8) waliomaliza muda wao (graduate) katika kiatamizi cha TEMDO wamewezeshwa kuendeleza miradi yao kibiashara wakiwa kama wapangaji wa TEMDO na mmoja (1) akiwa nje ya kiatamizi;

(iii) Kutayarisha andiko na mpango wa biashara (proposal and busines plan) kwa mradi wa kuzalisha umeme kwa mitambo inayoendeshwa kwa nguvu ya maji katika kijiji cha Mafuta-Mvomero Morogoro;

(iv) Kufanya maboresho makubwa katika teknolojia ya kuzalisha mkaa kutokana na mabaki ya mimea. Jumla ya mitambo mitatu (3) imetengenezwa ambapo mmoja (1) umefungwa huko Dodoma (1) na miwili (2) Arusha; na

(v) Kuboresha kiteketezi cha kuchomea taka za hospitali na taka ngumu (bio-medical solid waste incinerator) na kusimikwa katika hospitali tatu za Wilaya ya Siha, Mafia na Arusha.

**(c) Kwa upande wa zana za kilimo, CAMARTEC imetekeleza miradi ifuatayo:**

(i) Kubuni mashine ya kuvuna, kupura na kupepeta mpunga kwa maana ya kiasili [prototype] na kuifanyia majaribio katika eneo la Mabogini Mkoani Kilimanjaro;

(ii) Kuunda mashine za kufunga majani kwa ajili ya kuboresha matumizi ya malisho kwa kuongeza muda wa kukaa rafuni. Jumla ya mashine 16 zimetengenezwa na 10 zimesambazwa katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro;

(iii) Kuendelea kujenga mitambo mikubwa ya Biogasi kwa ajili ya kufua umeme kwenye shule na taasisi nchini. Katika mwaka 2013/2014, jumla ya vifaa 2,000 vya majiko ya biogesi vimekamilishwa na kusambazwa

katika Wilaya za Mwanga, Ilemela, Nyamagana, Dodoma na Singida;

(iv) Kuendelea kutoa mafunzo kwa watumiaji wa zana za kilimo ili kuongeza tija katika kilimo; na

(v) Taasisi za SIDO, TEMDO na CAMARTEC zimeendelea kushirikiana katika kubuni na kutengeneza teknolojia za kuongeza thamani. Teknolojia hizo ni pamoja na za kuongeza thamani mazao ya alizeti, muhogo, korosho, mahindi, soya, ngozi na mbogamboga.

**(d) SIDO imeendelea kutekeleza shughuli zifuatazo mwaka 2013/2014:-**

(i) Kwa kushirikiana na vituo vyake vya uendelezaji wa teknolojia vilivyopo Arusha, Iringa, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Mbeya na Shinyanga, iliwezesha utengenezaji wa zana mpya za aina 1,715 na kusambazwa kwa watumiaji. Teknolojia hizo zilihusisha ubanguaji wa korosho, usindikaji wa muhogo, usindikaji wa vyakula, upunguzaji wa matumizi ya miti na mazao yake kama nishati na ufungashaji wa vyakula vilivyosindikwa. Pia, zilihusu utengenezaji wa vifaa vya ujenzi hasa matofali, utengenezaji wa chokaa na chaki, ukamuaji mafuta ya kula, utengenezaji wa sabuni na usindikaji ngozi kwa kutumia njia za asili. Teknolojia hizo zimesaidia kuimarisha na kuongeza ubora wa bidhaa za wajasiriamali na hivyo kuziongezea ushindani katika soko; na

(ii) Pamoja nakukabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti, Wizara imewawezesha maofisa 94 wa

SIDO kupata mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi na hivyo kuwajengea uwezo wa kitaalam wa kuwahudumia wajasiriamali wadogo kwa ufanisi zaidi. Wizara iliweza kuwashawishi Washirika wa Maendeleo kutekeleza programu SIDO na pia kulijengea Shirika uwezo wa kuendeleza na kukuza jasiriamali ndogo na za kati nchini. Kwa sasa, kupitia SIDO, kuna miradi inayotekelezwa chini ya ufadhili wa IFAD, KOICA na wadau wengine wa MUVI (IFAD) na Vituo vya mafunzo ya Usindikaji wa Mazao (Training Cum Processing Centre)-KOICA.

## 2.9 USIMAMIZI WA SERA NA SHERIA KATIKA BIASHARA

***84. Mheshimiwa Spika,*** zoezi la awali la mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara kwa awamu ya kwanza ya kukusanya maoni ya wadau limekamilika. Aidha, awamu ya pili ni ya kufanya uchambuzi yakinifu wa maeneo mangine ili hatimaye kuendeleza kazi hiyo katika mwaka 2014/2015. Aidha, katika kipindi cha 2013/2014, Wizara imefanya maandalizi ya Sera ya Walaji (National Consumer Policy). Rasimu ya Sera hiyo imechambuliwa na kuwasilishwa katika ngazi za maamuzi.

***85. Mheshimiwa Spika,*** vilevile Wizara imekamilisha Rasimu ya Sera na Mkakati wa Kitaifa wa Miliki Ubunifu (National Intellectual Property Policy and Strategy) na maoni ya wadau yamezingatiwa katika uandaaji wa Sera na Mkakati wake. Mikutano ya kupata maoni ya wadau ilifanyika katika kanda tano ambazo ni: Kanda ya Mashariki Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kati na Kanda ya Kaskazini. Kinachofanyika sasa ni kuoanisha yaliyopo katika mkakati wa mwanzo na mapendekezo yaliyotolewa ili kuweza

kupata mkakati madhubuti kwa ajili ya hatua za ukamilishwaji wake.

***86. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, malengo ya Wizara katika masuala ya ushindani na udhibiti wa bidhaa na huduma kupitia TBS, TANTRADE, COSOTA, BODI YA MAGHALA, FCC, FCT na SIDO yalikuwa ni kuratibu ushindani, sera, kanuni za biashara na kusimamia ubora wa bidhaa na huduma; na kuthibitisha umahiri wa baadhi ya maabara.

***87. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Wakala wa Vipimo, utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo:

i. Ilirekebisha vipimo 8,336, na kaguzi 571 zilifanyika kwa ajili ya kuwalinda walaji;

ii. Kuanzisha vituo mbalimbali vya ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa mipakani na bandarini kama vile Sirari, Namanga, Horohoro, Holili, na Bandari ya Mwanza;

iii. Kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kama vile Magazeti, Redio na Luninga;

iv. Kuimarisha Kitengo cha Bandari kwa kupeleka watumishi tisa kwenye mafunzo ya upimaji wa mafuta na gesi (Oil and Gas metering), kuongeza vitendea kazi ikiwa ni pamoja na vifaa vya ofisi na vya usalama (safety gears), na kuongeza rasilimali watu ili kutoa huduma ya kusimamia vipimo bandarini kwa ufanisi zaidi;

v. Kuendelea kudhibiti usahihi wa vipimo vitumikavyo katika gesi asilia na ile itokanayo na mafuta ya petrol;

vi. Kujenga *Calibration Bay* ya kisasa katika eneo la Misugusugu mkoani Pwani mbapo tayari mchoraji amepatikana na anaendelea na kazi hiyo. Ujenzi wa *Calibration Bay* ya Mwanza umeanza na unatarajia kukamilika mwezi Mei, 2014 na Ujenzi wa *Calibration Bay* ya Iringa umekamilika na kituo kinafanya kazi.

***88. Mheshimiwa Spika,*** Msajili wa Makampuni ameendelea kujiimarisha ili kuboresha huduma zake. Wakala inaendelea na utaratibu wa kuweka mifumo ya kuwezesha usajili wa makampuni na majina ya biashara ili kufanyika kwa njia ya mtandao. Kazi hiyo inafanyika sambasamba na kuangalia, kuboresha taratibu za utendaji na kuweka mifumo na vifaa vya TEHAMA. Aidha, Sheria za Makampuni na Sheria ya Majina ya Biashara tayari zimefanyiwa marekebisho. Kanuni zake zimeandaliwa na kupitishwa na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara na tayari zinasubiri kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali ili zianze kutumika. Wakala imempata mtaalam elekezi kwa ajili ya kuchora jengo na kusimamia ujenzi katika Kiwanja Namba. 24 kilichopo maeneo ya *Ada Estate*,Wilaya ya Kinondoni. Ramani pamoja na taratibu za vibali na rasilimali fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi vinakamilishwa.

***89. Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Ushindani imeendelea kutekeleza jukumu lake la kuhakikisha ufanyaji biashara unaendeshwa kwa haki. Katika kufikia azma hiyo, Tume imetekeleza mambo yafuatayo:-

i. Kutekeleza kwa nguvu zaidi mpango wa kuteketeza bidhaa mbalimbali ambazo zimehifadhiwa kwenye

maghala mbalimbali ya Serikali kwa mujibu wa sheria za mazingira. Tume inawasiliana kwa karibu na Shirika la Mazingira la Taifa na Taasisi zingine ili kutafuta njia nzuri kimazingira ya kuteketeza bidhaa hizo. Tume imeweza kuwaadhibu waingizaji 186 wa bidhaa kutoka nje kwa kukiuka Sheria za Alama za Bidhaa;

ii. Kuandaa kongamano lililowakutanisha wamiliki wa nembo za biashara ili kuweka bayana utaratibu mzuri wa kushirikiana katika kupambana na kuthibiti bidhaa bandia katika soko la Tanzania;

iii. Kuthibiti bidhaa bandia katika mikoa mbalimbali kwa kufanya upekuzi wa ghafla mara 60 kwa lengo la kupambana na kuthibiti bidhaa bandia katika maduka na ghala mbalimbali za kuhifadhia bidhaa katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Moshi. Upekuzi huo ulihusishwa na ukiukaji wa Sheria za Alama za Bidhaa ambazo wamiliki wake waliwasilisha malalamiko. Bidhaa bandia zilizopekuliwa ni Konyagi, Nivea, IPS, Philips, A to Z, MEM, Gillette, Simba, Nokia, Tronics, Techno, Samsung na HP. Bidhaa bandia zimeendelea kukaguliwa na kudhibitiwa kwenye Bandari ya Dar es Salaam na Bandari za nchi kavu ambapo makontena 221 yalikamatwa. Bidhaa bandia zenye thamani ya Shilingi milioni 63 ziliweza kuteketezwa katika njia iliyo salama kimazingira;

iv. Kuchunguza masuala manne yanayokiuka Sheria ya Ushindani katika Sekta Ndogo za Saruji, Tumbaku, Gesi na Bima. Taarifa za uchunguzi katika masuala hayo zimewasilishwa sehemu husika na zipo kwenye hatua za mwisho za kusikilizwa na kufanyiwa uamuzi na Tume;

v. Kukamilisha utafiti wa ushindani katika masoko ya saruji na sukari kwa kushirikiana na Taasisi zinazosimamia ushindani katika nchi za Afrika Kusini, Botswana. Kenya, Namibia na Zambia. Tume pia inashiriki katika kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara inayofanya utafiti kuhusu changamoto za soko la saruji nchini;

vi. Kupokea na kuyashughulikia malalamiko 17, kati ya hayo, lalamiko moja linafanyiwa tathmini ya kisheria kwa kuangalia uzoefu wa nchi nyingine katika kufanya maamuzi juu ya matangazo potofu (deception and misleading on manufacturing process). Pamoja na hayo walalamikaji katika malalamiko 16 hawajaleta mrejesho na Tume inaendelea kufuatilia mwenendo wa malalamiko yanayohusu bidhaa husika ili kubaini endapo muuzaji/wauzaji wameacha mbinu hizo potofu baada ya kuelimishwa na Tume. Katika kipindi cha 2013/2014, bidhaa zilizolalamikiwa kwa kiwango kikubwa ni bidhaa za mawasiliano ambazo ni simu za viganjani na vipangusa (mobile phones na Ipad) na ubora wa mafuta ya alizeti yazalishwayo nchini; na

vii. Kuendelea na maandalizi ya rasimu ya Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji na iliweza kupitia mapendekezo ya wadau. Kazi ya kutengeneza sera imekwishaanza

***90. Mheshimiwa Spika***, taasisi nyingine iliyoko chini ya Wizara yangu inayohusika na usimamizi wa sheria na taratibu za kibiashara ni TBS. Katika mwaka 2013/2014, ilitekeleza mambo yafuatayo:

i. Kukagua na kuhakiki bidhaa kutoka nje ya nchi, ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2014, jumla ya vyeti 19,966 vya ubora wa bidhaa (Certificate of Conformity-

COC) zinazoingizwa kutoka nje vilitolewa kwa shehena za bidhaa mbalimbali. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2014, jumla ya magari 28,656 yalikaguliwa kupitia ukaguzi wa nje (Preshipment Verification) na jumla ya magari 51 yalikaguliwa baada ya kuingia nchini (Destination Inspection.). Aidha, Shirika linatarajia kufungua kituo kipya cha ukaguzi wa ubora wa bidhaa katika mpaka wa Tunduma. Faida kubwa ya utaratibu wa PVoC ni kuzuia bidhaa zisikokidhi ubora kuingizwa nchini na hivyo kuiepusha nchi kuwa jalala la bidhaa hafifu na kuondoa ushindani usio wa haki kati ya wafanyabiashara;

ii. Kufanya ukaguzi wa bidhaa zilizoko sokoni - katika mwaka 2013/2014 kuna bidhaa mbalimbali kwa mfano vilainishi vya injini (lubricants) vilivyoonekana havina ubora vilivyokuwa sokoni, hatua zilichukuliwa na kuufahamisha umma. Pia, zoezi la kuwachukulia hatua wazalishaji wanaopeleka bidhaa sokoni bila kuthibitishwa limekuwa endelevu na tumefanikiwa kuongeza maombi ya wazalishaji wanaotaka leseni za kutumia alama ya ubora ya TBS. Katika mwaka 2013/2014, bidhaa zilizopewa kipaumbele ni:

a) Mikate (bakery): Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Dodoma ambapo bakery 14 zilikaguliwa kwa kushitukizwa na kati ya hizo kumi (10) zimekwishapata leseni ya ubora. Zilizobaki bado ziko kwenye mchakato;

b) Nondo: Zoezi hilo liliendeshwa Tanzania nzima kwa wazalishaji wote wa nondo na viwanda 4 viligunduliwa kuzalisha bila kupata leseni ya ubora na kufungiwa kabla ya kuruhusiwa kuendelea na uzalishaji baada ya kupata leseni;

c) Maji: Wazalishaji kadhaa walitembelewa katika Mkoa wa Dar es Salaam na viwanda viwili vilisimamishwa kwa sababu ya kukiuka taratibu za leseni. Kiwanda kimoja kilichopo Dar es Salaam bado kimefungwa na kingine cha Tanga kimefunguliwa baada ya kutimiza masharti na;

d) Mitumba ya nguo za ndani: Zoezi hilo lilitiliwa mkazo na pia kutumia vyombo vya habari kuelimisha umma kuhusu madhara yake. Zoezi hilo lilifanyika kwa kukamata na kuteketeza nguo za ndani zilizokutwa katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya na Mwanza.

iii. Kuziwezesha maabara zake kupata vifaa vya kupimia kufikia viwango vya upimaji vya kimataifa. Hadi hivi sasa, jumla ya maabara nne (4) za Shirika la Viwango Tanzania zimehakikiwa na kupewa Vyeti vya Umahiri wa Utendaji wa Kazi zake. Maabara hizo ni pamoja na Maabara ya Ugezi (Metrology Laboratory), Maabara ya Chakula, Maabara za Kemia na Maabara ya Nguo/Ngozi.

iv. Kutoa mafunzo kwa wajasiriamali nchini katika mikoa ya Tabora, Shinyanga, Rukwa, Katavi na wilaya zote za Mkoa wa Dar- Es- Salaam. Mafunzo hayo yalianza rasmi mwezi Machi 2014**.**

## 2.10 UENDELEZAJI WA TAALUMA YA BIASHARA

***91. Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kimeendelea kutoa mafunzo ya elimu ya biashara kwa kada mbalimbali, kuanzia ngazi ya cheti hadi stashahada ya

uzamili katika fani za Uongozi wa Biashara, Uhasibu, Ugavi, Masoko, Mizani na Vipimo, Menejimenti ya Fedha, Rasilimali Watu, na Biashara za Nje (IBM). CBE imekamilisha maandalizi ya mitaala yenye uelekeo wa kiutendaji katika nyanja za biashara kuanzia ngazi ya cheti hadi shahada. Mitaala hiyo imeanza kutumika mwaka 2013/2014. Aidha, Chuo kipo katika jitihada za kuandaa mitaala mipya katika eneo la elimu ya biashara (Bachelor of Business Education). Chuo pia kimewapa wakufunzi wote mafunzo ya namna ya kuandaa na kuomba kazi za ushauri (consultancy services).

***92. Mheshimiwa Spika,*** katika kutafuta suluhu ya muda mfupi ya uhaba wa madarasa ya kufundishia, Chuo kimejenga darasa moja kubwa la muda katika Kampasi ya Dar es Salaam lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 likiwa na viti na feni. Katika mwaka 2013/2014, kulikuwa na jumla ya wahitimu 7,034 ambapo kati yao wanaume ni 3,554 na wanawake ni 3,480 walihitimu katika program mbalimbali. Chuo pia kimeingia mkataba na Chuo Kikuu cha Finland (University of Eastern Finland) kuendesha kwa pamoja Program za Degree za Uzamifu (PhD) ambapo wakufunzi watano wameanza masomo katika mwaka 2013/2014. Aidha, Chuo kwa kushirikiana na Uholanzi chini ya mradi wa NICHE kinatoa mafunzo ya uzamivu kwa wakufunzi wanne katika nchi mbalimbali.

## 3.0 MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

***93. Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Viwanda na Biashara ina watumishi wapatao 1,846 wa kada mbalimbali. Kati ya hao, watumishi 225 ni wa Wizarani na waliobaki 1,621 wapo katika Taasisi 18 za sekta hii. Kwa mwaka 2013/2014, Wizara imeajiri watumishi wawili wa kada ya Katibu

Mahsusi, imethibitisha kazini watumishi kumi na tisa (19) na kupandisha vyeo watumishi 47 wa kada mbalimbali waliokuwa na utendaji mzuri wa kazi na kukidhi mahitaji ya miundo yao ya kiutumishi. Aidha, Wizara imepeleka watumishi 45 kwenye mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuwajengea uwezo ili kuongeza ufanisi na tija katika utendaji wa kazi.

## 4.0 USIMAMIZI WA MAPATO NA MATUMIZI

***94. Mheshimiwa Spika,*** Katika kuimarisha usimamizi wa Mapato na Matumizi ya Serikali na kuhakikisha kwamba Sheria na Kanuni na taratibu za fedha zinazingatiwa, kwa mwaka 2013/2014, Wizara imefanya ukaguzi wa kawaida na kutoa taarifa za kila robo mwaka katika Kamati ya Ukaguzi ya Wizara. Pia, Wizara imekuwa ikitekeleza ushauri unaotolewa katika Taarifa za Ukaguzi ili kuhakikisha kwamba mapungufu yaliyobainishwa yanarekebishwa; imeratibu na kusimamia vikao vya Kamati ya Ukaguzi na Kamati ya Kusimamia na Kudhibiti Mapato na Matumizi ya Serikali na kuwasilisha taarifa katika ngazi husika kwa wakati. Wizara imesimamia na kujibu Hoja za Wakaguzi wa Nje na kushiriki katika vikao vya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC); Pia imeandaa na kuwasilisha Taarifa za Mwaka za Mapato na Matumizi kwa kufuata mfumo wa IPSAs na imeratibu na kuandaa Taarifa za Mapato na Matumizi na kuziwasilisha kwa wakati.

## 5.0 USIMAMIZI WA UNUNUZI

***95. Mheshimiwa Spika,*** Katika kutekeleza Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013, Wizara imeandaa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka 2013/2014 kulingana na Sheria hiyo na kusimamia utekelezaji wake.

## 6.0 HUDUMA ZA SHERIA

***96. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya mapitio na kurekebisha sheria mbalimbali zinazohusiana na masuala ya biashara kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini. Katika kipindi hichohicho, Wizara imetengeneza Kanuni sita za sheria zinazohusiana na ufanyaji wa biashara na tayari zipo hatua ya mwisho kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Aidha, Wizara inatarajia kufanya mapitio kwenye sheria zinazohusiana na biashara ambazo hazijafanyiwa mapitio. Wizara itaendelea na mashauri yaliyoko Mahakamani, na kwenye Tume na Mabaraza ya Uamuzi.

## 7.0 MAMBO MTAMBUKA

### (a) Kupambana na Rushwa

***97. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa watumishi wake kwa kutoa maelekezo mbalimbali ya sheria zinazotumika katika Utumishi wa Umma kupitia vikao vya kazi. Katika kuongeza uwajibikaji kwa wananchi, Wizara imehuisha Mkataba wa Huduma kwa Mteja kwa ajili ya kuboresha utendaji na kuongeza nguvu ya kuimarisha Dawati la Kushughulikia Malalamiko katika Sekta ya Viwanda na Biashara.

### (b) Kupambana na UKIMWI / VVU

***98. Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Waraka wa Serikali Na. 1 wa mwaka 2006, unaohusu huduma kwa watumishi wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi na wenye UKIMWI, Wizara

imeendelea kutoa huduma ya lishe, usafiri na virutubisho kwa watumishi wake waliojitokeza ili kuwaongezea afya waweze kuchangia katika ujenzi wa Taifa. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha upimaji wa afya za wafanyakazi kwa hiari na kusambaza vifaa vya kuzuia maambukizi kama vile mipira ya kiume na ya kike kwa watumishi wake na taasisi zake ili kupunguza maambukizi mapya.

### (c) Jinsia katika Sera, Mikakati, Programu za Wizara

***99. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2013/2014, Wizara imechukua hatua mbalimbali katika kujumuisha masuala ya jinsia katika sera, mikakati na programu za Wizara ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa maafisa bajeti 50 kutoka Wizarani na Taasisi zilizo chini yake. Mafunzo hayo yalihusiana na uchambuzi wa masuala ya jinsia katika bajeti. (Gender Responsive Budgeting). Aidha, mafunzo yalitolewa kwa Menejimenti ya Wizara jinsi ya kujumuisha masuala ya jinsia katika sera, mikakati, programu na bajeti ya Wizara.

***100. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetayarisha mwongozo kwa ajili ya uanzishwaji wa Dawati la Jinsia katika mipaka yote ya Tanzania ndani ya Jumuia ya Afrika Mashariki. Mwongozo umetoa ufafanuzi kuhusu mipaka na mamlaka ya madawati hayo na kuhakikisha kuwa rasilimali za kutosha zinapatikana. Aidha, kuhakikisha kuwa madawati yanakuwa na uwezo wa kutumikia wafanyabiashara wanawake na kufuatilia na kuripoti kuhusu utekelezaji wa sera zinazohusiana ya masuala ya jinsia katika Kamati za Pamoja Mipakani (Joint Border Commitees). Vilevile, Wizara kupitia Dawati la Jinsia linatarajiwa kuratibu na kupokea taarifa za madawati hayo moja kwa moja kutoka kwenye ofisi za mipakani, kuchambua, kuchukua hatua na kutoa ushauri kwa Kamati na sekta nyingine.

***101. Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliandaa semina ya uhamasishaji kwa Wasimamizi na Wafanyakazi wa Benki za Biashara na watoa huduma wengine wa Huduma za Fedha kwa lengo la kukuza upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya wanawake. Semina hizo zilifanyika Dar es Salaam, Morogoro na Tanga. Jumla ya taasisi 40 zilishiriki ikiwemo Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), CRDB Bank Ltd, Wanawake Bank, Twiga Bankorp Ltd, Azania Bank, National Microfinance Bank (NMB), Barclays, Standard Chartered, Stanbic Bank, Exim Bank, Benki ya Posta Tanzania (TPB), SIDO, PRIDE, Mhalili SACCOS, Bradec MFI, Tanga Wafanyakazi SACCOS, Diamond Trust Bank, Mkoa SACCOS, Bayport Tanzania Ltd, FINCA, Vision Fund Tanzania, na Ofisi ya Ustawi wa Jamii. Washiriki wa semina walibadilishana mawazo kuhusu changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo na walikubaliana kuwa kuna umuhimu wa kuwa na dirisha tofauti kwa wanawake.

## 8.0 CHANGAMOTO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA

***102. Mheshimiwa Spika,*** Katika utekelezaji wa malengo yake, Sekta ya Viwanda na Biasha imekabiliwa na changamoto kuu ya uhaba wa rasilimali fedha, kukabiliwa na mlolongo mkubwa wa kodi, ushuru na tozo mbalimbali. Changamoto zingine zinazokabili sekta hii ni gharama kubwa za kufanya biashara (cost of doing bussiness) zinazotokana na kupanda kwa bei ya umeme na maji, teknolojia duni za uzalishaji na uhaba wa *technicians* (specialised industrial skills personnel) katika fani mbalimbali viwandani ambako kumeendelea kuwa ni changamoto kwa sekta.

***103. Mheshimiwa Spika,*** Maeneo mengine yenye kuleta changamoto ni ushindani usio wa haki unaotokana na kuingizwa kwa bidhaa kutoka nje ambazo hazijalipiwa ushuru

stahiki, ukosefu wa maeneo ya kutosha yaliyotengwa kwa uwekezaji wa viwanda na ukosefu wa mitaji ya kuanzisha viwanda imezidi kurudisha nyuma jitihada za kuendeleza viwanda nchini.

## 9.0 MALENGO YA MWAKA 2014/2015

## 9.1 SEKTA YA VIWANDA

***104. Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka 2014/2015, Sekta ya Viwanda ina malengo yafuatayo:-

i) Kuendelea na utekelezaji wa Mkakati Unganishi wa Uendelezaji Viwanda Nchini kwa kuhamasisha uwekezaji na kutoa vipaumbele kwa viwanda vinavyoongeza thamani mazao ya kilimo;

ii) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya Mchuchuma na Liganga, TANCOAL, Kasi Mpya, umeme wa upepo mkoani Singida na kiwanda cha kuzalisha viuadudu vya kuulia viluwiluwi wa mbu waenezao malaria;

iii) Kufuatilia uendelezaji na uwekezaji katika maeneo ya EPZ na SEZ ikiwemo ulipaji wa fidia kwa maeneo husika;

iv) Kuendelea kutoa mafunzo ya kuongeza tija, ufanisi na ubora wa bidhaa kwa wenye viwanda kupitia Program za Kaizen, pamoja na uimarishaji na uboreshaji viwanda (*Industrial Upgrading and Modernization*) na utafiti katika mifumo ya ubunifu (*national systems of innovation survey*) kwa kushirikiana na JICA na UNIDO mtawalia;

v) Kuendelea kushiriki katika uhamasishaji wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa Sera ya Viwanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sera ya Viwanda kwa nchi za SADC na Nguzo ya Maendeleo ya Eneo huru la Biashara la Utatu linalojadiliwa;

vi) Kufuatilia ufufuaji wa viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo havifanyi kazi na ufufuaji wa Viwanda vya *General Tyre* na Urafiki;

vii) Kukamilisha Sheria ya Kusimamia Biashara ya Chuma Chakavu na kuandaa kanuni zake;

viii) Kuendeleza utekelezaji wa Mkakati wa Kuendeleza Viwanda vya Ngozi na Bidhaa za Ngozi;

ix) Kuendeleza utekelezaji wa Mkakati wa Kuendeleza Viwanda vya Nguo na Mavazi;

x) Kufanya Sensa ya viwanda nchini kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu;

xi) Kuendelea kuhamasisha, kuhifadhi na kulinda mazingira katika shughuli zote za uzalishaji viwandani;

xii) Kufanya tathmini ya maendeleo ya viwanda ili kubaini changamoto zinazokabili sekta na kuzitafutia ufumbuzi;

xiii) Kurejea Mpango Kabambe wa Kuendeleza Viwanda;

xiv) Kuandaa *catalogue* yenye taarifa mbalimbali za kusaidia wawekezaji;

xv) Kurejea sheria iliyoanzisha Shirika la Maendeleo la Taifa kwa kushirikiana na NDC;

xvi) Kurejea sheria zilizoanzisha taasisi za utafiti wa viwanda na maendeleo za CAMARTEC, TIRDO na TEMDO; na

xvii) Kuandaa *framework* ya kuhawilisha teknolojia zinazobuniwa na taasisi za utafiti.

## 9.2 SEKTA YA VIWANDA VIDOGO NA BIASHARA NDOGO

***105. Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka 2014/2015, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ina malengo yafuatayo:-

i) Kupitia na kutathimini utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo;

ii) Kuwezesha upatikanaji wa maeneo ya kufanyia kazi kwa wajasiriamali;

iii) Kuwezesha jasiriamali ndogo na za kati kupata huduma za kifedha na zisizo za kifedha;

iv) Kuwezesha upatikanaji wa teknolojia za uongezaji thamani katika bidhaa kwa wajasiriamali wadogo na wakati;

v) Kuwezesha wajasiriamali wadogo na wakati kupata masoko ya bidhaa zao ndani na nje ya nchi; na

vi) Kuendelea kusimamia Mradi wa Muunganisho Ujasiriamali Vijijini (MUVI).

## 9.3 SEKTA YA BIASHARA

***106. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2014/2015, Sekta ya Biashara ina malengo yafuatayo:

i) Kuendeleza majadiliano kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa kwa lengo la kupanua wigo wa fursa za masoko yenye masharti nafuu;

ii) Kuendeleza majadiliano ya Ubia wa Uchumi kati ya Jumuiya ya Ulaya na Jumuiya ya Afrika Mashariki;

iii) Kuendeleza majadiliano ya kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara la Utatu (*Tripartite Free Trade Area-FTA);*

iv) Kushiriki hatua ya pili ya majadiliano ya kuanzisha Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC Monetary Union);*

v) Kuendelea na majadiliano ya kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha wa SADC *(SADC Customs Union)* na kulegezeana masharti katika biashara ya huduma *(Trade in Services Liberalization);*

vi) Kuendelea kuimarisha Kamati ya Kitaifa inayoshughulikia ufuatiliaji, utoaji taarifa na utekelezaji wa Mikakati ya Kuondoa Vikwazo vya Biashara Visivyokuwa vya Kiushuru (NTBs);

vii) Kuendelea kufuatilia na kushiriki majadiliano ya Duru la Doha kwa lengo la kutetea maslahi ya Tanzania; na

viii) Kuendelea na majadiliano kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Marekani (USA) kuhusu Ubia wa Biashara na Uwekezaji.

## 9.4 SEKTA YA MASOKO

***107. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 201/2015, malengo ya Sekta ya Masoko ni yafuatayo:-

i) Kuendelea kushirikiana na wadau ili kuendeleza miundombinu ya masoko nchini;

ii) Kuimarisha mazingira ya kufanya biashara mipakani;

iii) Kukamilisha marekebisho ya sheria zinazokinzana na uboreshaji wa mazingira ya biashara;

iv) Kuandaa Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji (National Consumer Protection Policy);

v) Kushirikiana na wadau kukamilisha maandalizi ya kuanzisha Soko la Mazao na Bidhaa (Commodity Exchange market);

vi) Kuendeleza Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani ili uweze kutumika katika uanzishaji wa Soko la Mazao na Bidhaa (Commodity Exchange);

vii) Kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza taarifa za masoko kwa wadau kwa wakati;

viii) Kuhamasisha matumizi ya fursa za masoko ya mipakani, kikanda na kimataifa; na

ix) Kutangaza bidhaa za Tanzania katika masoko ya ndani na nje.

x) Kuandaa Sera ya Taifa ya Viwango (National Standards Policy);

xi) Kukamilisha maandalizi ya Mradi wa Business Portal;

xii) Kuanzisha Mfumo wa Utoaji wa Leseni za Biashara kwa Njia ya elektroniki; na

xiii) Kukamilisha maandalizi ya Sera na Mkakati wa Miliki Ubunifu (Intellectual Property Policy & Strategy).

## 9.5 TAASISI CHINI YA WIZARA

### 9.5.1 Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kuzalisha Bidhaa za Kuuza Nje (EPZA)

***108. Mheshimiwa Spika,*** Malengo ya EPZA kwa mwaka 2014/2015 ni yafuatayo:-

i) Ulipaji wa fidia kwenye maeneo yaliyofanyiwa uthamini katika Bagamoyo SEZ, Kigoma SEZ Tanga SEZ , *Tanzania China Logistics Centre* na Ruvuma SEZ;

ii) Uendelezaji wa miundombinu ya msingi katika maeneo ya SEZ yaliyolipiwa fidia eneo la Bagamoyo SEZ, *Tanzania China Logistics Centre*, Bunda SEZ, Mererani SEZ na Manyara SEZ;

iii) Kunadi (Promotion) miradi/maeneo ya SEZ za Bagamoyo, Bunda na Mererani kwa wawekezaji

### 9.5.2 Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)

***109. Mheshimiwa Spika,*** Malengo ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) katika mwaka 2014/2015 ni kama ifuatavyo:-

i) Kuendeleza utekelezaji wa Miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga;

ii) Kukamilisha ujenzi wa Kiwanda cha Kuzalisha Viuadudu (biolarvicides) vya Kuua Viluwiluwi wa Mbu Waenezao Malaria katika eneo la TAMCO, Kibaha;

iii) Kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Ngaka Kusini, Songea;

iv) Kukamilisha upatikanaji wa mkopo wa Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia upepo mkoani Singida na kuanza ujenzi;

v) Kukarabati Kiwanda cha *General Tyre*, Arusha ili kukifufua na kuanza uzalishaji wa matairi;

vi) Kukamilisha tafiti na kuanzisha Kiwanda cha Kuzalisha Magadi Soda eneo la Ziwa Natron na Engaruka, Arusha;

vii) Kuanzisha viwanda vya kusindika nyama, mpira na mazao mengine ya Kilimo;

viii) Kuendeleza utekelezaji wa Mradi wa Kasi Mpya wa Kuzalisha Chuma Ghafi;

ix) Kujenga maeneo ya viwanda (Industrial parks) sehemu za TAMCO, KMTC na Kange;

x) Kuwajengea uwezo wananchi wa maeneo husika kufaidi miradi inayotekelezwa na NDC; na

xi) Kuratibu uendelezaji wa Kanda za Maendeleo za Mtwara, Tanga, Kati na Uhuru.

### 9.5.3 Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC)

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** malengo ya CAMARTEC kwa mwaka 2014/2015 ni yafuatayo:-

i) Kubuni na kutengeneza teknolojia za kuongeza tija na kupungauza harubu (drudgery) katika kilimo na ufundi vijijini;

ii) Kubuni na kutengeneza teknolojia za kuboresha usafiri na uchukuzi vijijini;

iii) Kuendeleza utafiti na kuboresha mashine ya kuvuna na kupura mpunga (rice combine harvester);

iv) Kubuni na kutengeneza mashine ya kutengeneza matofali inayoendeshwa kwa injini;

v) Kuendelea kurekebisha sheria iliyoanzisha CAMARTEC ili kukidhi matakwa mapya;

vi) Kuendelea kuunda mashine ya kufunga majani kwa ajili ya kuboresha matumizi ya malisho kwa kuongeza muda wa kukaa rafuni;

vii) Kuendelea kujenga mitambo mikubwa ya biogesi kwa ajili ya kufua umeme kwenye shule na taasisi nchini kwa kuanzia na Mikoa ya Manyara, Mara Kagera na Mwanza;

viii) Kuendelea kueneza vifaa vya matumizi ya nishati ya biogesi (biogas appliances) katika maeneo kulikojengwa mitambo ya biogesi ili kuifanya teknolojia hiyo kuwa endelevu;

ix) Kuendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali juu ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na usanifu wa mitambo ya biogesi; na

x) Kuendelea kutoa mafunzo kwa watumiaji wa zana za kilimo ili kuongeza tija katika kilimo.

### 9.5.4 Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (TEMDO)

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** Malengo ya **TEMDO** katika mwaka 2014/2015 ni yafuatayo:-

i) Kubuni, kuendeleza na kuhamasisha utengenezaji kibiashara (commercialization) wa mitambo/teknolojia za:- Kuzalisha umeme kutokana na nguvu ya maji (micro hydro-power plant) kwa matumizi ya uzalishaji wa umeme vijijini; Kusindika na kusafisha mafuta yatokanayo na mbegu za mimea (oil expelling and refining plant); Kuteketeza taka za hospitali (medical solid waste incinerator); Jokofu la kuhifadhia vifaa vya hospitali pamoja na maiti (refrigeration systems for medical use including mortuary facility); na kutengeneza kuni au mkaa utokanao na mabaki ya mimea (biomass briquetting plant);

ii) Kufanya utafiti ili kubaini mahitaji ya teknolojia na huduma za kihandisi katika viwanda na sekta nyingine nchini. Vilevile, kufanya utafiti wa kubaini uwezo na uwezekano wa kutengeneza vifaa vya pikipiki nchini;

iii) Kuboresha miundombinu ya kiatamizi na kutoa huduma kwa wajasiriamali watengenezaji wa mashine

na vifaa kwa matumizi ya viwanda vidogo na vya kati (machinery and equipment for light industries)na

iv) Kutoa huduma ya ushauri wa kihandisi pamoja na mafunzo katika viwanda kumi (10) vya kati na vikubwa kwa lengo la kuongeza uzalishaji, ukuaji wa biashara, ubora wa bidhaa na uendeshaji wa faida.

### 9.5.5 Taasisi ya Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO)

***112.*** ***Mheshimiwa Spika,*** malengo ya TIRDO kwa mwaka 2014/2015 ni ifuatavyo:-

i) Kufanya tafiti zenye lengo la kupata teknolojia bora za uzalishaji na zenye tija kwa viwanda;

ii) Kufanya utafiti na kutoa mafunzo ya utunzaji siri (Cyber Security) katika Taasisi za serikali na Wakala wa Serikali ;

iii) Kuendelea kufuatilia na kutekeleza Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi (land use plan) baada ya mpango huo kuwa umepitishwa na kuidhinishwa na Serikali;

iv) Kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Kuimarisha Sekta ya Ngozi na Viwanda vya Ngozi ili kupunguza uharibifu wa mazingira kwa kurejesha taka za ngozi ili kutengeneza bidhaa kama *leather boards;*

v) Kuendelea na ukamilisha wa mchakato wa kuhakiki (Accreditation) na kuboresha maabara ya mazingira na ya vifaa vya kihandisi ili ziweze kufikia viwango

vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani;

vi) Kuendelea kutekeleza Mfumo wa Ufuatiliaji wa Mazao (traceability) kwa kutumia TEKNOHAMA na pia kusaidia utendaji wa Kampuni ya GS1 (TZ) National Ltd kama mshauri wa kiufundi kwani uendeshaji wa GS 1 ni wa Sekta Binafsi;

vii) Kuendelea kukamilisha mchakato wa kurejea Sheria ya Bunge namba 5 ya mwaka 1979 iliyoanzisha TIRDO kwa kuwasilisha ripoti ya mapitio ya sheria kwa Wizara mama;

viii) Kuendelea kutoa tathmini za kitaalam kwa wawekezaji wakubwa na wadogo kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo (TIB) pamoja na benki nyinginezo; na

ix) Kuendelea kutoa huduma za kitaalamu viwandani zenye lengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora bila kuchafua mazingira pia zinazolenga matumizi bora ya nishati.

### 9.5.6 Shirika la Viwango Tanzania (TBS)

***113. Mheshimiwa Spika,*** malengo ya Shirika la Viwango kwa mwaka 2014/2015 ni yafuatayo:-

i) Kuendeleza utekelezaji wa utaratibu wa kupima ubora wa bidhaa zote mahali zinapotoka kabla ya kuingia nchini (Preshipment Verification of Conformity to Standards – PVoC);

ii) Kushirikiana kwa karibu na vyombo vingine vya Serikali kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA), Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Tume ya Ushindani (FCC) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinazoingia nchini ni zenye ubora unaokubalika;

iii) Kuongeza idadi ya leseni kutoka leseni 100 zinazotarajiwa kwa mwaka 2013/2014 na kufikia leseni 120 katika mwaka 2014/2015;

iv) Kuongezeka idadi ya upimaji sampuli kutoka 10,000 kwa mwaka hadi kufikia 11,000 katika mwaka 2014/2015;

v) Kutayarisha viwango vya kitaifa vinavyofikia 150 vikiwemo viwango vya Sekta ya Huduma katika mwaka 2014/2015;

vi) Kuendelea na juhudi za kuhakikisha kwamba maabara zote za Shirika zinapata vyeti vya umahiri (laboratory accreditation) ili kuongeza kukubalika kwa bidhaa nyingi za Tanzania katika soko la ndani na la kimataifa;

vii) Kuendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali nchini kote kuhusu viwango vya udhibiti wa ubora wa bidhaa na kuongeza vyeti vya ubora wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje kwa mwaka 2014/2015; na

viii) Kuendelea kuimarisha utaratibu wa kukagua ubora wa bidhaa ukiwemo ukaguzi wa magari kabla kuingia nchini.

### 9.5.7 Baraza la Ushindani (FCT)

***114. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Baraza litatekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kusikiliza kesi za rufaa zinatokana na mchakato wa Udhibiti na Ushindani wa Biashara kwenye soko;

b) Kujenga uwezo zaidi wa Baraza katika kushughulika kesi hizo kwa kuimarisha rasilimali watu na Wajumbe wa Baraza;

c) Kutoa elimu kwa umma juu ya kazi za Baraza na umuhimu wake katika uchumi; na

d) Kuimarisha upatikanaji wa rasilimali fedha ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza.

### 9.5.8 Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)

***115. Mheshimiwa Spika,*** malengo ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni kwa mwaka 2014/2015 ni yafuatayo:-

i) Kuendelea na maandalizi ya utaratibu wa kuweka mifumo ya kiteknolojia itakayowawezesha wadau kupata taarifa na huduma kwenye mifumo ya kompyuta (On line registration systems) kwa wakati;

ii) Kuboresha usajili wa makampuni na majina ya biashara kwa kutumia mfumo na mashine za kisasa '*special machine readable certificates*';

iii) Kufanya marejeo ya sheria zinazosimamiwa na Wakala ili ziweze kwenda na wakati;

iv) Kuboresha mifumo ya uwekaji na utunzaji wa masijala tano za kisheria zinazosimamiwa na Wakala ili kuweza kushabihiana na mifumo ya kiteknolojia na hatimaye kurahisisha utoaji huduma;

v) Kuendelea kuelimisha umma kuhusu shughuli za Wakala na umuhimu wa kusajili biashara;

vi) Kuendeleza watumishi na kuwawekea mazingira mazuri ya utendaji kazi ili kuongeza tija na uwajibikaji;

vii) Kuendeleza uhusiano na mashirika ya kimataifa ambayo Tanzania ni mwanachama;

viii) Kuanza kwa ujenzi wa Jengo la BRELA kwa ajili ya Ofisi na Masijala;

ix) Kutoa huduma za usajili kwa wateja wa BRELA kwa mtindo wa papo kwa hapo katika maonesho mbalimbali kama Sabasaba, Nanenane, Wiki ya Utumishi wa Umma, makongamano na katika warsha zinazoandaliwa na Wakala au Wadau wengine kama SIDO, MKURABITA na wengineo pindi fursa zinapotokea;

x) Kuendeleza na kuimarisha mahusiano mazuri na ushirikiano na taasisi mbalimbali za ndani ya nchi katika kufanikisha shughuli za Wakala; na

xi) Kuendeleza na kuimarisha ushirikiano na taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi ambazo ni wadau wa taarifa mbalimbali zinazotunzwa na Wakala.

### 9.5.9 Tume ya Ushindani (FCC)

***116. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Tume imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i) Kudhibiti na kupambana na uingizaji na uzalishaji wa bidhaa bandia;

ii) Uchunguzi na usikilizaji wa kesi za ushindani;

iii) Utafiti wa masoko ili kubaini matatizo ya ushindani usio wa haki wa masoko husika na hatua za kurekebisha; na

iv) Kumlinda na kumwelimisha mlaji.

### 9.5.10 Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji (NCAC)

***117. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha 2014/2015, Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji litatekeleza yafuatayo:-

i) Kusimamia maslahi ya mlaji kwa kupeleka maoni yake kwenye Tume ya Ushindani, Mamlaka za Udhibiti na Serikali kwa ujumla;

ii) Kuendelea kupokea na kusambaza taarifa na maoni yenye maslahi kwa mlaji; na

iii) Kuanzisha Kamati za Mlaji za Mikoa na Sekta na kushauriana na Kamati hizo, wenye viwanda, Serikali na jumuiya nyingine za walaji katika mambo yenye maslahi kwa mlaji.

### 9.5.11 Bodi ya Leseni ya Maghala (TWLB)

***118. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Bodi ya Maghala itatekeleza yafuatayo:-

i) Kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Maghala katika maeneo yote yanayotekeleza mfumo huo hapa nchini;

ii) Kutoa elimu ya Mfumo kwa wadau hususan wakulima waishio vijijini;

iii) Kujenga uwezo kwa wakulima na wadau wengine wa mfumo kwa kuwapa mafunzo ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani;

iv) Kuratibu shughuli za wadau wa Mfumo wa Stakabadhi za Maghala;

v) Kuwaunganisha wakulima na taasisi za fedha kupitia Vikundi na Vyama vya Ushirika ili waweze kupata mikopo; na

vi) Kuiwakilisha Serikali kwenye mikutano na makongamano ya kitaifa na kimataifa yanayojadili masuala yanayohusiana na Mfumo wa Stakabadhi za Maghala.

### 9.5.12 Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO)

***119. Mheshimiwa Spika,*** malengo ya SIDO kwa mwaka 2014/2015 ni yafuatayo:-

i) Kujenga uwezo wa vituo vya maendeleo ya teknolojia vya SIDO kuzalisha mashine ndogo zitakazotumika katika uongezaji thamani mazao ya kilimo hasa vijijini;

ii) Kuhakikisha teknolojia za uongezaji thamani wa mazao yaliyochaguliwa chini ya Mkakati wa Bidhaa Moja kwa kila Wilaya (ODOP) kama alizeti, ngozi, asali na korosho, zinazalishwa na kusambazwa kwa watumiaji;

iii) Kutoa elimu ya ujasiriamali, usimamizi wa biashara na usindikaji wa vyakula;

iv) Kuwawezesha wazalishaji wadogo kupata masoko ya bidhaa na huduma zao, kwa kutengeneza miundombinu ya kupokea na kusambazia habari za kibiashara, kutengeneza sehemu za kuonyeshea bidhaa za wazalishaji wadogo;

v) Kutoa huduma za kifedha ikiwa ni pamoja na ushauri na mikopo pale itakapojidhihirisha kuhitaji;

vi) Kuendelea kuchangia katika gharama za utekelezaji wa mradi wa kuendeleza ujasiriamali vijijini (MUVI); na

vii) Kuimarisha mfumo wa TEHAMA wa SIDO.

### 9.5.13 Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA)

***120.*** ***Mheshimiwa Spika,*** malengo ya COSOTA kwa mwaka 2014/2015 ni yafuatayo:-

i) Kufungua Ofisi ya Kanda ya Hakimiliki mjini Arusha kwa ajili ya Kanda ya Kaskazini na mjini Dodoma kwa ajili ya Kanda ya Kati na Magharibi;

ii) Kukamilisha marejeo ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ya mwaka 1999;

iii) Kuanza utaratibu wa kusambaza stika (Hakigram) kwa wasambazaji wote wa kazi za muziki na filamu;

iv) Kuhamasisha wanunuzi wa CD, kanda za miziki na filamu kununua kanda na CD zenye Hakigram; na

v) Kuingia mkataba na makampuni binafsi kwa lengo la kukusanya mirabaha na kufanya operesheni dhidi ya kazi bandia.

### 9.5.14 Mamlaka ya Biashara Tanzania (TanTrade)

***121.*** ***Mheshimiwa Spika,*** malengo ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania kwa mwaka 2014/2015 ni yafuatayo:-

i) Kuwajengea uwezo wajasiriamali ili waweze kuzijua fursa na changamoto za masoko ya ndani na nje na jinsi ya kuzimudu;

ii) Kuwawezesha wanawake wafanyabiashara kwenye sekta isiyo rasmi katika mipaka ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (Trade facilitation for Women Informal Cross-Border Traders in the East Africa Community),

ambayo ni mipaka ya Kabanga, Mutukula, Sirari na Namanga;

iii) Kukuza biashara na kutafuta masoko ya ndani kwa kuratibu Maonesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF, 2014);

iv) Kutafuta masoko ya nje kwa kuratibu Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya nchi za nje;

v) Kuwaunganisha wafanyabiashara na wadau wengine na fursa mbalimbali zikiwemo masoko ya ndani na nje ya nchi, kuwapa uelewa wa mwenendo wa bei za bidhaa Kitaifa na Kimataifa;

vi) Kuendeleza Soko la Ndani kwa kusisimua maendeleo ya biashara katika sekta muhimu za kiuchumi;

vii) Kutoa huduma ya taarifa za kibiashara;

viii) Kushiriki katika kuboresha mfumo na sera za biashara; na

ix) Kuimarisha Ofisi ya Zanzibar.

### 9.5.15 Wakala wa Vipimo (WMA)

***122. Mheshimiwa Spika,*** malengo ya Wakala wa Vipimo kwa mwaka 2014/2015 ni yafuatayo:-

i) Kuendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi ya vipimo vilivyo sahihi nchini kupitia uimarishwaji wa uhakiki na ukaguzi wa vipimo hivyo kwa lengo kuu la kumlinda mlaji;

ii) Kuendelea kuongeza mbinu za utoaji wa elimu ya matumizi ya vipimo hivyo kwa umma ili kuongeza

uelewa wa matumizi yake na ufungashaji wa bidhaa kwa kiasi sahihi ili mnunuzi aweze kupata bidhaa hiyo kulingana na thamani ya fedha yake;

iii) Kuendelea kuimarisha Kitengo cha Vipimo Bandarini (WMA Pots Unit) chenye jukumu la kusimamia, kuhakiki na kukagua usahihi wa vipimo vitumikavyo kupimia kiasi cha mafuta yaingiayo hapa nchini ili kiweze kutoa huduma hiyo kwa ufanisi;

iv) Kukamilisha kazi ya utafiti na uchambuzi wa mfumo wa vipimo vitumikavyo katika usambazaji wa gesi asilia (Natural Gas) ili kuweza kukamilisha zoezi la utengenezaji wa Kanuni za Gesi hiyo itakayokidhi usimamizi wa matumizi sahihi ya vipimo hivyo;

v) Kuendelea na zoezi la kuandaa kanuni mpya ya ufungashaji wa gesi kwenye mitungi itokanayo na mafuta ya petroli (LPG) kwa kuwashirikisha zaidi wadau ili kuwezesha usimamizi wa usahihi wa kiasi cha gesi inayowekwa kwenye mitungi hiyo;

vi) Kuendelea na kazi ya ujenzi wa kituo cha kupimia magari yanayosafirisha mafuta katika eneo la Misugusugu - Pwani, Kituo cha Mwanza na Iringa;

vii) Kuendelea na taratibu za kukamilisha utungaji wa Sheria Mpya ya Vipimo (Legal Metrology Act) ili kukidhi matakwa ya sasa ya biashara na pia kuzingatia maridhiano yaliyofikiwa na nchi kikanda na kimataifa kuhusu masuala ya vipimo; na

viii) Kuendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa kuongeza vitendea kazi ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya kitaalam na vyombo vya usafiri imara na vya kutosha

kwa ofisi zote ili kuhakikisha huduma za Wakala zinazowafikia walaji/wadau wengi zaidi, kwa haraka na ufanisi zaidi.

### 9.5.16 Kituo cha Biashara cha Tanzania Dubai-(TTC-Dubai)

***123.*** ***Mheshimiwa Spika,*** malengo ya Kituo cha Biashara cha Tanzania Dubai-(TTC-Dubai) kwa mwaka 2014/2015 ni yafuatayo:

i) Kushirikiana na TAHA pamoja na TANTRADE, kuandaa ziara ya kuuza (Selling Mission) kwenda mjini Dubai ili kukutana na wanunuzi wa Matunda na Mboga Mboga (Fresh Fruits and Vegetables) na bidhaa zingine kama maparachichi, mananasi, vitunguu, *fresh beans*, *capsicum* na *baby carrot*;

ii) Kuratibu na kufadhili kwa kiasi ushirika wa makampuni ya Tanzania kwenye Maonesho ya Chakula (Gulf Food) yatakayofanyika mwezi Februari, 2015. Bidhaa lengwa ni pamoja na korosho zilizobanguliwa, kahawa na chai, asali, viungo na *pulses*;

iii) Kwa kushirikiana na wadau wa *Real Estates*, Kituo kitaandaa kongamano la uwekezaji kwenye *Real Estates* nchini UAE; na

iv) Kuratibu na kufadhili kwa kiasi ushiriki wa makampuni ya Tanzania yaliyopo kwenye Sekta ya Mbao kushiriki maonesho ya Dubai *Wood Show* yatakayofanyika Februari, 2015.

### 9.5.17 Kituo cha Biashara cha Tanzania London

***124. Mheshimiwa Spika,*** malengo ya Kituo cha Biashara cha Tanzania London-(TTC-London) kwa mwaka 2014/2015 ni yafuatayo:-

a) Kukuza biashara kwa kushiriki kwenye mikutano ya mashirika ya Kimataifa ambayo Tanzania ni nchi mwanachama. Mashirika hayo ni:- Shirika la Kimataifa la Kahawa Duniani (International Coffee Organisation - ICO), Shirika la Kimataifa la Nafaka – IGC, Shirika la Kimataifa la Sukari – ISO na Shirika la Katani – LSA. Vilevile, kushiriki maonesho ya kibiashara yatakayofanyika London ambayo ni kama yale ya kahawa na asali;

b) Kwa kushirikiana na Ubalozi, kuandaa mikutano kuhusu kuvutia uwekezaji katika Sekta za Kilimo, Miundombinu, Huduma na Utalii;

c) Kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania kupitia maonesho mbalimbali ya utalii yatakayofanyika katika miji mikubwa ya Uingereza, kama vile Manchester, Birmingham, London, Glasgow na Dublin; na

d) Kukuza Diplomasia ya Uchumi kwa kushiriki katika shughuli za mashirika ya Kimataifa ili kubaini fursa za kibiashara na kiuchumi. Mashirika hayo ni kama vile, Shirika la Utafiti wa Kilimo duniani, Umoja wa Wafanyabiashara wa Kitanzania nchini Uingereza (UK Tanzania Business Group), Shirika la Kahawa, Katani, Sukari, pamoja na lile la Nafaka.

### 9.5.18 Chuo Cha Elimu ya Biashara (CBE)

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Chuo Cha Elimu ya Biashara kinalenga kutekeleza yafuatayo:

a) Kuandaa mitaala mipya katika taaluma ya usimamizi wa nishati ya mafuta na gesi, ujasiriamali na elimu ya biashara pamoja na mitaala mipya katika ngazi ya shahada ya umahiri (Masters Degree);

b) Kuimarisha uwezo wa wakufunzi (capacity building) katika mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya shahada za umahiri na uzamivu;

c) Kuanzisha ujenzi wa Kampasi ya Mwanza katika kiwanja cha Kiseke kwa kuzingatia *master plan*;

d) Kuboresha miundombinu ya Kampasi ya Dar es Salaam na Dodoma; na

e) Kutafuta eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya Mbeya na kuandaa *master plan* yake.

### 10.0 SHUKRANI

***126. Mheshimiwa Spika,*** Naomba kuwashukuru kwa dhati Nchi Rafiki na Mashirika ya Kimataifa ambayo yamekuwa yakitoa na yanaendelea kutoa misaada mbalimbali kwa Sekta ya Viwanda na Biashara. Misaada na michango hiyo imekuwa chachu na nyenzo muhimu kwa Wizara yangu kuweza kutekeleza majukumu yake. Nchi rafiki ni pamoja na Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Sweden, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Mashirika ya Kimataifa ni pamoja na: Benki ya Dunia, DANIDA, CFC, ARIPO, DFID, EU, FAO, IFAD, JICA, Jumuiya ya Madola, KOICA, Sida, UNCTAD, UNDP, UNIDO, USAID, WTO na WIPO.

# 11.0 MAOMBI YA FEDHA KATIKA MWAKA 2014/2015

## 11.1 MAPATO YA SERIKALI

***127. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara inatarajia kukusanya Shilingi **5,204,719,000** kutokana na ada za leseni, uuzaji wa nyaraka za zabuni, faini kwa kukiuka sheria ya leseni na makusanyo mengine.

## 11.2. MAOMBI YA FEDHA

***128. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara ya Viwanda na Biashara imeomba kutengewa jumla ya shilingi **112,497,801,000** kutekeleza majukumu ya kuindeleza Sekta. Kati ya fedha hizo, Shilingi **33,656,090,000** ni za Matumizi ya Kawaida na Shilingi **78,841,711,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

### 11.2.1 Matumizi ya Kawaida

***129. Mheshimiwa Spika,*** kati ya Shilingi **33,656,090,000** fedha za Matumizi ya Kawaida, Shilingi **26,215,350,000** zimetengwa kwa ajili ya Mishahara (PE) na Shilingi **7,440,740,000** zimetengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Kati ya Shilingi **7,440,740,000** zilizotengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), Shilingi **2,081,287,600** zitatokana na makusanyo ya ndani ya Wizara. Aidha, katika Shilingi **7,440,740,000** zilizotengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, Shilingi **6,154,820,000** ni kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Shilingi **1,285,920,000** ni kwa ajili ya matumizi ya Taasisi zilizo chini ya Wizara.

### 11.2.2 Matumizi ya Fedha za Maendeleo

**i. Fedha za Ndani**

***130. Mheshimiwa Spika,*** katika bajeti ya Shilingi **78,841,711,000** iliyotengwa kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo, Shilingi **74,000,000,000** ni fedha za ndani na Shilingi **4,841,711,000** ni fedha za nje kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Miradi itakayotekelezwa ni kama vile *Tanzania Mini Tiger Plan* 2020 Shilingi **7,000,000,000** zimetengwa kulipia fidia eneo la Bagamoyo SEZ; Shilingi **53,000,000,000** kulipia fidia eneo la *Tanzania China Logistics Center* - Kurasini; Mchuchuma Coal Shilingi **2,000,000,000** zitatumika kuendeleza utekelezaji wa miradi ya Kasi Mpya na Makaa ya Mawe ya Mchuchuma; Shilingi **3,000,000,000** zitatumika kutekeleza Mradi wa Chuma cha Liganga na Shilingi **2,030,000,000** zimetengwa kwa ajili ya *ASDP* kuchangia katika utekelezaji wa miradi ya Sekta ya Kilimo inayojumuisha uanzishaji wa Soko la Mazao na Bidhaa. Aidha, *NDC-Malaria Project* imetengewa Shilingi **2,906,000,000** ili kukamilisha ujenzi wa Kiwanda cha Kuzalisha Viuadudu (biolarvicides) vya Kuua Viluwiluwi wa Mbu Waenezao Malaria.

**ii. Fedha za Nje**

***131. Mheshimiwa Spika,*** bajeti ya Shilingi **4,841,711,000** ya fedha za Maendeleo za Nje zitatumika katika kutekeleza miradi ya maeneo mbalimbali ifuatayo ya sekta:

a) *Rural Micro, Small and Medium Enterprises Support Programme* (MUVI) umetengewa Shilingi **1,615,237,000**

b) *Support for Trade Mainstreaming* umetengewa Shilingi ***1,210,500,000***.

c) *Support for Gender Mainstreaming in Trade Sector and Micro and Small Enterprise Development Strategy* umetengewa Shilingi **624,107,000**

d) *Strengthening TWLB Capacity for efficiency in Warehouse Receipt System (WRS) service provision in Tanzania* umetengewa Shilingi **203,967,000**

e) *BEST PROGRAMME* umetengewa Shilingi **1,187,900,000**

## 11.0 HITIMISHO

***132. Mheshimiwa Spika,*** napenda kukushukuru tena wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia kwenye tovuti ya Wizara www.mit.go.tz.

***133. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

# VIAMBATISHO

**Jedwali Na. 1: Vigezo vya Ufanisi Katika Sekta ya Viwanda**

| Mwaka | Mchango katika Pato la Taifa (%) (Bei za 2001) | Ukuaji wa Sekta (Bei za 2001) | Mchango katika Mauzo nje (%) | Mchango katika Mauzo nje yasiyo Asilia (%) | Ongezeko la mauzo nje ya bidhaa za viwanda (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1998 | 8.37 | 5.5 | 6.10 | 15.40 | - |
| 1999 | 8.47 | 6.0 | 5.50 | 12.40 | -15.7% |
| 2000 | 8.46 | 4.8 | 6.50 | 11.71 | 44.2% |
| 2001 | 8.38 | 5.0 | 7.23 | 9.05 | 29.4% |
| 2002 | 8.40 | 7.5 | 7.40 | 8.52 | 17.3% |
| 2003 | 8.57 | 9.0 | 6.79 | 8.42 | 27.2% |
| 2004 | 8.69 | 9.4 | 8.28 | 9.37 | 31.4% |
| 2005 | 8.87 | 9.6 | 9.31 | 11.81 | 41.8% |
| 2006 | 9.02 | 8.5 | 11.24 | 13.81 | 25.4% |
| 2007 | 9.15 | 8.7 | 15.28 | 18.14 | 57.9% |
| 2008 | 9.36 | 9.9 | 20.73 | 28.48 | 139.9% |
| 2009 | 9.54 | 8.0 | 15.36 | 21.35 | -31.7% |
| 2010 | 9.61 | 7.9 | 22.29 | 30.34 | 90.3% |
| 2011 | 9.74 | 7.8 | 16.90 | 22.99 | -10.6% |
| 2012 | 9.85 | 8.2 | 17.61 | 24.91 | 20.4% |
| 2013 | 9.92 | 7.7 | 20.04 | 28.34 | 3.3% |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha

## Jedwali Na 2: Uzalishaji wa Baadhi ya Bidhaa Viwandani

| | | | | | | | | | | | | | | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Aina ya Bidhaa | Kipimo | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012** | 2013* | 2012-2013 |
| Biskuti & tambi | Tani | 2,284 | 5,906 | 10,214 | 10,912 | 10,565 | 11,273 | 15,435 | 15,200 | 7,435 | 12,053 | 16,383 | 17,440 | 6.5% |
| Unga wa ngano | Tani | 219,118 | 355,616 | 338,076 | 368,019 | 434,160 | 406,336 | 287,925 | 368,885 | 444,242 | 439,926 | 443,731 | 516,778 | 16.5% |
| Konyagi | 000 Lita | 2,937 | 3,670 | 4,105 | 4,489 | 5,365 | 5,622 | 4,049 | 10,201 | 11,186 | 15,432 | 16,774 | 20,680 | 23.3% |
| Bia | 000 Lita | 175,870 | 194,100 | 202,628 | 216,604 | 299,036 | 310,194 | 291,178 | 284,906 | 242,689 | 323,393 | 339,605 | 374,238 | 10.2% |
| Chibuku | 000 Lita | 19,400 | 14,825 | 10,119 | 11,106 | 11,559 | 10,320 | 10,235 | 16,141 | 21,037 | 23,474 | 22,028 | 19,935 | -9.5% |
| Sigara | Milioni | 3,778 | 3,920 | 4,219 | 4,445 | 5,095 | 5,821 | 6,101 | 5,831 | 6,181 | 6,630 | 7,558 | 7,710 | 2.0% |
| Nguo | (000) $M^2$ | 106,305 | 116,714 | 111,637 | 99,134 | 146,600 | 139,000 | 140,531 | 91,501 | 103,177 | 101,820 | 83,592 | 86,639 | 3.6% |
| Kamba za katani | Tani | 5,901 | 6,839 | 5,161 | 5,943 | 5,854 | 7,012 | 7,783 | 7,913 | 6,872 | 6,976 | 7,441 | 6,908 | -7.2% |
| Nyavu za uvuvi | Tani | 30 | 41 | 260 | 274 | 119 | 156 | - | 64 | 247 | 164 | 295 | 297 | 0.7% |
| Mazulia | (000) $M^2$ | - | - | - | - | - | - | - | 37,152 | - | - | - | - | |
| Tabaka za mbao | Cu.m | 304 | 32,609 | 40,248 | 37,941 | 44,310 | 45,147 | 44,547 | 266 | - | 30,589 | 37,005 | 41,106 | 11.1% |
| Dawa za pareto | Tani | 36 | 16 | 23 | 25 | 33 | 33 | 73 | - | 49 | 53 | 73 | 113 | 54.8% |
| Mbolea | Tani | - | - | - | - | - | - | - | 25,762 | - | 11,200 | - | - | |
| Rangi | 000 Lita | 13,564 | 16,842 | 16,621 | 16,222 | 18,402 | 17,451 | 24,857 | - | 28,201 | 31,211 | 34,942 | 36,623 | 4.8% |
| Bidhaa za petrol | 000 Tani | - | - | - | - | - | - | - | 1,941 | - | - | - | - | |
| Saruji | 000 Tani | 1,026 | 1,186 | 1,281 | 1,366 | 1,422 | 1,630 | 1,756 | 34,793 | 2,313 | 2,409 | 2,581 | 2,346 | -9.1% |
| Chuma | Tani | 25,418 | 38,794 | 41,710 | 41,299 | 44,482 | 52,163 | 39,969 | 34,793 | 33,384 | 39,955 | 46,323 | 46,148 | -0.4% |
| Bati | Tani | 31,742 | 31,018 | 29,573 | 29,737 | 29,898 | 36,492 | 31,743 | 50,664 | 71,276 | 76,912 | 78,677 | 73,787 | -6.2% |
| Aluminium | Tani | 141 | 199 | 171 | 183 | 105 | 110 | 105 | 58 | 59 | 33 | 71 | 40 | -43.7% |
| Radio | 000 Na. | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | |
| Betri | Milioni | 42 | 43 | 74 | 81 | 82 | 75 | 53 | 78 | 93 | 89 | 69 | 75 | 8.7% |

- Hakuna uzalishaji;
** Zimerekebishwa (Revised)
* Za Awali (Provisional)

Chanzo: Ofisi za Takwimu na Wizara ya Viwanda na Biashara 2013

## Jedwali Na. 3: Thamani ya Bidhaa Zilizouzwa Nje

## (Miln USD)

| JUMUIYA/ NCHI | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013p | 2012 -2013 (Badiliko) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **JUMUIYA YA ULAYA** | 461.9 | 440.0 | 464.0 | 553.5 | 745.4 | 898.4 | **20.5%** |
| **NCHI NYINGINE ZA ULAYA** | 533.3 | 469.0 | 687.1 | 828.5 | 816.8 | 16.9 | **-97.9%** |
| **JUMLA - BARA LA ULAYA** | **995.2** | **909.0** | **1151.1** | **1382.0** | **1562.2** | **915.3** | **-41.4%** |
| **JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)** | | | | | | | |
| Afrika ya kusini | 232.5 | 170.9 | 416.8 | 831.1 | 967.9 | 760.5 | **-21.4%** |
| Zambia | 36.6 | 44.3 | 53.5 | 47.1 | 71.4 | 90.6 | **26.9%** |
| Swaziland | 0.6 | 20.8 | 0 | 12.5 | 2.2 | 4.1 | **86.4%** |
| Zimbabwe | 1.2 | 5.7 | 0 | 4.1 | 4.7 | 6.5 | **38.3%** |
| Msumbiji | 31.4 | 20.3 | 17.7 | 61.9 | 53.1 | 66.4 | **25.0%** |
| Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 124 | 79.9 | 137.1 | 119.5 | 181.6 | 236.2 | **30.1%** |
| Nchi nyingine za SADC | **17.1** | **32.3** | **0** | **82.6** | **141** | **44.9** | **-68.2%** |
| **JUMLA- SADC** | **443.4** | **374.2** | **625.1** | **1158.8** | **1421.9** | **1209.2** | **-15.0%** |
| **JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)** | | | | | | | |
| Burundi | 19.5 | 23.6 | 51.0 | 30.8 | 45.8 | 45.0 | **-1.7%** |
| Kenya | 235 | 177.4 | 297.3 | 211.2 | 330.9 | 227.1 | **-31.4%** |
| Rwanda | 20.6 | 15.1 | 55.0 | 65.8 | 72.8 | 81.1 | **11.4%** |
| Uganda | 40.5 | 47.7 | 46.8 | 44.6 | 65.8 | 66.1 | **0.5%** |
| **JUMLA – EAC** | **315.6** | **263.8** | **450.1** | **352.4** | **515.3** | **419.3** | **-18.6%** |
| **Nchi nyingine za Afrika** | **96.1** | **0.6** | **5.8** | **67.9** | **47.7** | **3.5** | **-92.7%** |
| **JUMLA –AFRIKA** | **855.1** | **638.6** | **1081.0** | **1579.1** | **1984.9** | **1632.0** | **-17.8%** |
| **BARA LA AMERIKA** | | | | | | | |
| Marekani | 55.1 | 39.5 | 46.5 | 47.5 | 66.8 | 60.5 | **-9.4%** |
| Canada | 3.8 | 6.1 | 4.6 | 5.0 | 25.2 | 12.9 | **-48.8%** |
| Nchi nyingine za Bara la Amerika | 5.4 | 0 | 0 | 7.4 | 1.7 | 2.7 | **58.8%** |
| **JUMLA- BARA LA AMERIKA** | **64.3** | **45.6** | **51.1** | **59.9** | **93.7** | **76.1** | **-18.8%** |
| **ASIA** | | | | | | | |
| China | 223.5 | 363.9 | 634.2 | 659.2 | 520.4 | 307.8 | **-40.9%** |
| India | 171.8 | 183.8 | 218.5 | 202.7 | 476.5 | 748.2 | **57.0%** |
| Japan | 136.9 | 164.7 | 209.7 | 346.8 | 296.5 | 220 | **-25.8%** |
| Umoja wa Falme za Kiarabu | 65.4 | 66.8 | 55.3 | 74.9 | 94.2 | 84.2 | **-10.6%** |
| Hong Kong | 13.4 | 85.6 | 12.6 | 11.1 | 23.1 | 30.4 | **31.6%** |
| Singapore | 11.0 | 6.4 | 13.5 | 10.9 | 24.3 | 55.7 | **129.2%** |
| **Nchi nyingine za Asia** | 52.4 | 59.1 | 56.4 | 109.1 | 209.4 | 64.7 | **-69.1%** |
| **JUMLA- ASIA** | **674.4** | **930.3** | **1200.2** | **1414.7** | **1644.4** | **1511** | **-8.1%** |
| **NCHI NYINGINEZO** | **989.8** | **774.6** | **840.9** | **662.2** | **604.0** | **1214.5** | **101.1%** |
| **JUMLA KUU** | **3,578.8** | **3,298.1** | **4,324.3** | **5,097.9** | **5,889.2** | **5,348.9** | **-9.2%** |

Chanzo: Benki Kuu na Wizara ya Fedha

**Jedwali Na. 4: Wastani wa Bei za Mazao Makuu ya Chakula 2006/2007 hadi 2013/2014 (Mwenendo wa Bei ya Mazao ya Chakula Tsh/100Kg)**

| Mazao | 2006/7 | 2007/8 | 2008/9 | 2009/10 | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 | % Mabadiliko (2013/- Machi 2014) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 18,047 | 31,727 | 37,298 | 42,133 | 34,247 | 43,308 | 65,028 | 55,854 | (14.11) |
| Maharage | 57,365 | 90,670 | 107,152 | 105,092 | 109,537 | 122,868 | 131,337 | 129,957 | (1.05) |
| Mchele | 57,779 | 90,670 | 97,213 | 99,790 | 99,721 | 152,799 | 172,654 | 132289 | (23.4) |
| Ngano | 38,056 | 69,435 | 71,342 | 79,823 | 73,694 | 75,968 | 95,196 | 101,094 | 6.20 |
| Uwele | 26,441 | 41,424 | 46,033 | 47,451 | 51,512 | 75,442 | 73,085 | 84,413 | 15.50 |
| Ulezi | 35,137 | 57,806 | 61,477 | 72,593 | 71,819 | 75,442 | 105,453 | 122,607 | 16.27 |
| Mtama | 23,810 | 45,673 | 46,617 | 58,270 | 51,850 | 59,878 | 70,370 | 79,894 | 13.53 |

**Chanzo:** Wizara ya Viwanda na Biashara, 2014

**Jedwali Na.5: Thamani, Kiasi na Bei ya Bidhaa Zilizouzwa Nje (2009-2013)**

| Bidhaa | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | Badiliko |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa Asilia** | | | | | | |
| **Kahawa** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 111.2 | 101.6 | 142.6 | 186.6 | 171.0 | -8.4% |
| Kiasi ('000 tani) | 56.0 | 35.6 | 39.0 | 54.8 | 59.5 | 8.5% |
| Bei (US$ kwa tani) | 1984.6 | 2853.1 | 3654.9 | 3403.2 | 2872.7 | -15.6% |
| **Pamba** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 111.0 | 84.0 | 61.6 | 164.9 | 111.7 | -32.3% |
| Kiasi ('000 ttani) | 99.4 | 67.6 | 40.3 | 132.0 | 89.0 | -32.6% |
| Bei (US$ kwa tani) | 1116.7 | 1241.9 | 1529.0 | 1249.7 | 1256.0 | 0.5% |
| **Katani** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 6.7 | 10.9 | 16.9 | 18.4 | 16.9 | -7.8% |
| Kiasi ('000 tani) | 8.2 | 11.6 | 13.8 | 13.5 | 12.6 | -6.8% |
| Bei (US$ kwa tani) | 826.0 | 939.8 | 1223.5 | 1357.1 | 1341.6 | -1.1% |
| **Chai** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 47.2 | 49.8 | 47.2 | 56.1 | 56.9 | 1.5% |
| Kiasi ('000 tani) | 30.6 | 27.1 | 27.1 | 27.2 | 28.8 | 5.8% |
| Bei (US$ kwa tani) | 1538.7 | 1840.2 | 1739.7 | 2061.2 | 1977.9 | -4.0% |
| **Tumbaku** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 127.4 | 232.4 | 281.2 | 350.1 | 307.0 | -12.3% |
| Kiasi ('000 tani) | 33.8 | 53.6 | 73.3 | 105.6 | 67.8 | -35.7% |
| Bei (US$ kwa tani) | 3764.0 | 4337.0 | 3839.4 | 3316.0 | 4526.1 | 36.5% |
| **Korosho** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 68.6 | 96.9 | 107.0 | 142.6 | 162.4 | 13.9% |
| Kiasi ('000 tani) | 95.5 | 100.6 | 96.4 | 130.9 | 147.3 | 12.5% |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Bei (US$ kwa tani) | 718.2 | 963.2 | 1110.0 | 1089.3 | 1102.5 | 1.2% |
| **Karafuu** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 14.4 | 7.6 | 28.9 | 38.1 | 43.0 | 12.8% |
| Kiasi ('000 tani) | 4.8 | 2.2 | 2.2 | 3.4 | 4.1 | 19.6% |
| Bei (US$ kwa tani) | 2977.9 | 3449.6 | 13162.9 | 11198.5 | 10562.8 | -5.7% |
| **Jumla (Bidhaa Asilia)** | **486.4** | **583.2** | **685.5** | **956.7** | **868.9** | **-9.2%** |
| **Bidhaa Zisizo Asilia** | | | | | | |
| **Madini** | **1274.8** | **1561.2** | **2283.4** | **2197.8** | **1861.2** | **-15.3%** |
| Dhahabu | 1229.5 | 1516.6 | 2224.1 | 2117.4 | 1732.9 | -18.2% |
| Almasi | 18.9 | 11.1 | 10.2 | 30.2 | 39.8 | 31.5% |
| Madini mengine | 26.4 | 33.5 | 49.2 | 50.2 | 88.5 | 76.3% |
| **Bidhaa za Viwandani** | **506.5** | **964.0** | **861.5** | **1037.3** | **1072.1** | **3.3%** |
| Nyuzi za Pamba | 8.1 | 11.5 | 4.8 | 5.8 | 10.9 | 88.8% |
| Kahawa Iliyozalishwa | 2.0 | 0.7 | 1.1 | 1.0 | 1.1 | 7.1% |
| Tumbaku ilizalishwa | 7.0 | 10.5 | 16.7 | 24.6 | 32.2 | 30.7% |
| Mazao ya Katani | 13.4 | 9.0 | 11.8 | 9.1 | 9.7 | 6.3% |
| Mazao mengine ya Viwandani | 476.1 | 932.4 | 827.1 | 996.8 | 1018.2 | 2.1% |
| **Samaki na Mazao ya Samaki** | **155.0** | **150.4** | **137.7** | **160.6** | **130.6** | **-18.7%** |
| **Mazao ya mboga na Maua** | **33.3** | **30.8** | **36.4** | **31.3** | **28.1** | **-10.2%** |
| **Bidhaa zilizouzwa tena (re-exports)** | **282.9** | **338.2** | **330.2** | **555.7** | **517.6** | **-6.8%** |
| **Bidhaa nyinginezo** | **120.4** | **132.5** | **98.3** | **181.7** | **172.8** | **-4.9%** |
| **Jumla (Bidhaa zisizo Asilia)** | **2372.9** | **3177.0** | **3747.5** | **4164.4** | **3782.3** | **-9.2%** |
| Bidhaa zisizorekodiwa | 438.9 | 564.0 | 664.9 | 768.2 | 697.7 | -9.2% |
| **JUMLA KUU (BIDHAA ZOTE)** | **3298.1** | **4324.3** | **5097.9** | **5889.2** | **5348.9** | **-9.2%** |
| Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha | | | | | | |

**Jedwali Na. 6: Wastani wa Bei ya Mazao kwa Mkulima kwa Mazao ya Biashara 2007/2008 hadi 2013/2014 (Bei/Kg)**

| Mazao | 2007/2008 | 2008/2009 | 2009/2010 | 2010/2011 | 2011/2012 | 2012/2013 | 2013/2014 | Mabadiliko 2012/13 Machi 2014 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Chai | 98 | 112 | 120 | 126 | 196 | 206 | 226 | 9 |
| Kahawa Arabica* | 1,600 | 1,750 | 1,700 | **3,350** | **3,903** | **2750** | 2250 | (18) |
| Kahawa Robusta | 500 | 800 | 450 | 900 | 941 | 1300 | 1100 | (15) |
| Mkonge | 796 | 771 | 888 | 921 | 1,114 | 1249.8 | 1370 | 9 |
| Pamba | 450 | 480 | 440 | 650 | 1,000 | 1200 | 700 | (41) |
| **Korosho** | 610 | 675 | 700 | 800 | 1,200 | 1000 | 800 | (20) |

**Chanzo:** Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

## Jedwali Na. 7:Mwenendo wa Bei za Mifugo Tanzania (2009 – 2013)

| **Ng'ombe** | | **2009** | **2010** | **2011** | **2012** | **2013** | **Mabadiliko 2012/2013** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Majike | Daraja la II | 331,077 | 343,402 | 383,496 | 424,683 | 426,071 | 0.33 |
| | Daraja la III | 249,433 | 249,550 | 305,339 | 338,833 | 320,180 | (5.51) |
| Madume | Daraja la II | 448,316 | 444,305 | 471,382 | 536,252 | 553,148 | 3.15 |
| | Daraja la III | 321,507 | 321,169 | 350,963 | 395,953 | 396,464 | 0.13 |
| Madume+Majike | Daraja III | 285,470 | 285,359 | 328,151 | 367,393 | 358,322 | (2.47) |
| Madume+Majike | Daraja II | 389,696 | 393,853 | 427,438 | 480,467 | 489,609 | 1.90 |
| **Mbuzi** | | | | | | | |
| Majike | Daraja la II | 39,853 | 40,455 | 45,338 | 49,907 | 50,801 | 1.79 |
| | Daraja la III | 29,098 | 29,860 | 34,392 | 35,872 | 35,332 | (1.51) |
| Madume | Daraja la II | 46,446 | 48,782 | 54,618 | 59,201 | 59,628 | 0.72 |
| | Daraja la III | 34,438 | 36,126 | 39,309 | 41,325 | 41,580 | 0.62 |
| Madume+Majike | Daraja la II | 43149.45 | 44,618.58 | 49,978 | 54,554 | 55,214 | 1.21 |
| Madume+Majike | Daraja la III | 31768.1 | 32,992.94 | 36,850 | 38,598 | 38,456 | (0.37) |
| Madume+Majike | Daraja (II+III) | 37458.78 | 38,805.76 | 42,323 | 46,576 | 46,835 | 0.56 |
| **Kondoo** | | | | | | | |
| Majike | Daraja la II | 33,239 | 35,183 | 39,804 | 40,887 | 43,743 | 6.99 |
| | Daraja la III | 26,660 | 26,540 | 29,966 | 31,179 | 30,095 | (3.47) |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Madume | Daraja la II | 39,883 | 43,955 | 47,654 | 48,486 | 51,150 | 5.49 |
| | Daraja la III | 30,924 | 31,656 | 34,353 | 33,378 | 34,864 | 4.45 |
| Madume+Majike | Daraja la II | 36,561 | 39,569 | 43,729 | 44,686 | 47,446 | 6.18 |
| Madume+Majike | Daraja (III) | 28,792 | 29,098 | 32,160 | 32,278 | 32,480 | 0.62 |
| Madume+Majike | Daraja (II+III) | 29,767 | 32,677 | 37,078 | 37,132 | 39,303 | 5.85 |

**Chanzo:** Wizara ya Viwanda na Biashara